SHERIA YA USHAHIDI, 2016

MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU **MAELEZO**

SEHEMU YA KWANZA
VIFUNGU VYA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kutumika.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UHUSIANO WA MATUKIO

4. Ushahidi unaoweza ukatolewa kwa matukio yanayobishaniwa na matukio yanayohusiana.
5. Uhusiano wa matukio yanayofanya sehemu ya tukio lile lile.
6. Matukio ambayo kutokea kwake, sababu au athari za matukio yanayobishaniwa.
7. Dhamira, maandalizi na hisia za kabla au baada.
8. Matukio ambayo ni muhimu kueleza au kutambulisha matukio husika.
9. Vitu vilivyosemwa au kufanywa na mlanjama wakiwa na dhamira moja.
10. Wakati ambao matukio hayahusiani vyenginevyo huwa yanahusika.
11. Katika mashauri yanayohusiana na fidia hoja zitakazoiwezesha Mahakama kutoa maamuzi ya kiwango zinahusika.
12. Hoja zinazohusika pale ambapo haki au desturi zinajadiliwa.
13. Matukio yanayoonesha uwepo wa hali ya ufahamu wa kiakili au kimwili au hisia za kimwili.
14. Hoja zinazojadiliwa ama tendo limefanyika kwa bahati mbaya au kwa kukusudia
15. Kuwepo kwa sababu za kutendeka kwa jambo ambalo linahusika

SEHEMU YA TATU
KUKUBALI

16. Maana ya kukubali.
17. Kukubali kwa mdaawa katika kesi au wakala wake au upande wenye maslahi.
18. Kukubali kwa watu ambao nafasi zao lazima zithibitishwe dhidi ya mdaawa katika dai.
19. Kukubali kwa watu ambao moja kwa moja wametajwa na mdaawa katika dai.

20. Uthibitisho wa kukubali dhidi ya watu waliotoa maelezo hayo ya kukubali na au kwa niaba yao.
21. Wakati ambao kukubali kwa mdomo juu ya yaliyomo katika nyaraka ni yenye kukubalika.
22. Wakati ambao kukubali kwa mdomo kwa yaliyomo katika kumbukumbu za kielektroniki kunakubalika.
23. Ni wakati gani kukubalika katika kesi za madai kunakubalika.
24. Kukubali sio uthibitisho kamili lakini kunaweza kuzuia.

SEHEMU YA NNE
MAUNGAMO

25. Ni wakati gani ungamo lililosababishwa na ushawishi, kitisho au ahadi, haihusiani katika mwenendo wa jinai.
26. Ungamo mbele ya Hakimu.
27. Ungamo la mshtakiwa akiwa katika udhibiti wa Polisi halitathibitika dhidi yake.
28. Kiasi cha taarifa ambazo zimepokelewa kutoka kwa mshtakiwa zinaweza kuthibitishwa.
29. Ungamo lililofanywa baada ya kuondolewa hisia zilizosababishwa na ushawishi, kitisho au ahadi, zinahusiana.
30. Ungamo ambalo vyenginevyo lisingehusika kwa sababu ya ahadi ya usiri.
31. Zingatio la ungamo lililothibitika linamuathiri mtu aliyeungama na watu aliounganishwa nao katika kesi kwa kosa moja.

SEHEMU YA TANO
MAELEZO YA WATU AMBAO HAWAWEZI KUITWA KAMA MASHAHIDI

32. Maelezo ya watu ambao hawawezi kuitwa kama mashahidi.
33. Kukubalika kwa kumbukumbu za biashara.
34. Uthibitisho wa maelezo ya maandishi katika mienendo ya jinai.
35. Uthibitisho wa maelezo ya kimaandishi katika mwenendo wa madai.
36. Uhusiano wa baadhi ya ushahidi kwa kuthibitisha kesi zilizotokea baada, ukweli wa matukio yaliyotajwa.

SEHEMU YA SITA
MAELEZO YALIYOFANYWA KWENYE MAZINGIRA MAALUM

37. Maingizo katika vitabu vya mahesabu yanapohusiana.
38. Uhusiano wa ingizo katika kumbukumbu za umma zilizofanywa katika kutekeleza majukumu.

39. Uhusiano wa maelezo kwenye ramani, michoro na mipango.
40. Uhusiano wa maelezo juu ya matukio ya umma yaliyomo katika sheria fulani, gazeti au taarifa.
41. Uhusiano wa maelezo kwa sheria yoyote iliyomo katika vitabu vya sheria.
42. Ushahidi uliopatikana kwa njia ya siri.
43. Namna ya maelezo yanayotakiwa kuthibitishwa.

SEHEMU YA SABA
HUKUMU ZA MAHAKAMA WAKATI ZINAPOHUSIKA

44. Hukumu zilizopita zinahusika katika kuzuwia shauri la pili au kusikiliza.
45. Uhusiano wa hukumu fulani katika baadhi ya kesi za madai.
46. Uhusiano na athari za hukumu, amri, au amri baada ya hukumu, zisizokuwa zile ambazo zimetajwa katika kifungu cha 45.
47. Hukumu zisizokuwa zile zilizotajwa katika kifungu cha 44 na 45 namna zinavyohusika.
48. Udanganyifu, au kula njama katika kupatikana kwa hukumu.

SEHEMU YA NANE
MAONI YA MTU WA TATU YANAPOHUSIKA

49. Maoni ya wataalamu.
50. Mambo yanayozingatiwa katika maoni ya wataalamu.
51. Maoni ya maandishi ya mkono yanapohusika.
52. Pale ambapo maoni yanayohusiana uwekaji saini kidigitali yanapohusika.
53. Maoni ya uwepo wa haki au desturi yanapohusika.
54. Maoni yanayohusiana na matumizi ya imani yanapohusika.
55. Maoni ya mahusiano yanapohusika.
56. Sababu za maoni zinapohusika.

SEHEMU YA TISA
WAKATI TABIA ZINAPOHUSIKA

57. Katika mashauri ya madai kuthibitisha hisia zilizoshutumiwa haihusiani.
58. Katika kesi za jinai, tabia njema za wakati uliopita zinahusiana.
59. Tabia mbaya za wakati uliopita hazihusiani, isipokuwa katika majibu.
60. Tabia zinazoathiri fidia.

SEHEMU YA KUMI
MATUKIO AMBAYO HAYAHITAJI KUTHIBITISHWA

61. Matukio yanayotambuliwa na Mahakama hayahitaji kuthibitishwa.
62. Matukio ambayo yanapaswa kutambuliwa na Mahakama.
63. Matukio yaliyokubaliwa hayahitaji kuthibitishwa.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
USHAHIDI WA MDOMO

64. Uthibitisho wa matukio kwa ushahidi wa mdomo.
65. Ushahidi wa mdomo lazima uwe wa moja kwa moja.
66. Ushahidi wa mikutano ya video au njia nyengine.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
USHAHIDI WA WARAKA

67. Uthibitisho wa maudhui ya nyaraka.
68. Ushahidi halisi.
69. Ushahidi usiokuwa halisi.
70. Uthibitisho wa nyaraka kwa ushahidi halisi.
71. Kesi ambazo ushahidi usio halisi unaohusiana na nyaraka unaweza kutolewa.
72. Masharti maalum yanayohusiana na kumbukumbu za kielektroniki.
73. Kukubalika kwa kumbukumbu za kielektroniki.
74. Taratibu za notisi ya kutoa hati.
75. Kuthibitishwa saini na mwandiko wa mtu anayedaiwa kusaini au kutolewa waraka ulioandikwa.
76. Uthibitisho wa saini ya kidigitali.
77. Uthibitisho wa kusainiwa waraka unaohitaji kushuhudiwa kisheria.
78. Uthibitisho pale ambapo shahidi aliyeshuhudia hapatikani.
79. Kukubalika kwa saini ya mtu aliyeshuhudia waraka.
80. Uthibitisho ambapo shahidi aliyeshuhudia anakanusha kutiwa saini.
81. Uthibitisho wa waraka ambao hautakiwi kisheria kushuhudiwa.
82. Ulinganisho wa saini, muandiko au muhuri na vyengine uliokubalika au kuthibitishwa.
83. Uthibitisho juu ya usahihi wa saini ya Kidigitali.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
NYARAKA ZA UMMA

84. Nyaraka za Umma.
85. Nyaraka binafsi.
86. Nakala za nyaraka za Umma zilizothibitishwa.
87. Uthibitisho wa Nyaraka kwa kutoa hati zilizothibitishwa.
88. Uthibitisho wa Nyaraka nyengine Rasmi.

SEHEMU YA KUMI NA NNE
DHANA JUU YA NYARAKA

89. Dhana juu ya uhalali wa nakala zilizothibitishwa.
90. Dhana juu ya nyaraka zinazotolewa kama kumbukumbu ya ushahidi.
91. Dhana juu ya Gazeti rasmi la serikali, magazeti, sheria za baraza la kutunga sheria na Nyaraka nyenginezo.
92. Dhana kuhusiana na Gazeti rasmi katika mfumo wakielektroniki.
93. Dhana kuhusiana na ukusanyaji wa sheria na ripoti za maamuzi.
94. Dhana kuhusiana na ramani au michoro iliyofanywa na mamlaka ya Serikali.
95. Dhana kuhusiana na nyaraka binafsi zilizofanywa nje ya Zanzibar.
96. Dhana kuhusiana na hati ya uwakala.
97. Dhana juu ya makubaliano ya kielektroniki.
98. Dhana juu ya kumbukumbu za kielektroniki.
99. Vyeti vya saini ya kidigitali.
100. Dhana kuhusiana na nakala zilizothibitishwa za kumbukumbu za Mahakama ya kigeni.
101. Dhana kuhusiana na vitabu, ramani na michoro.
102. Dhana kuhusiana na ujumbe wa mawasiliano ya simu.
103. Dhana kuhusiana na ujumbe wa kielektroniki.
104. Dhana kuhusiana na utiaji saini wa nyaraka zisizotolewa.
105. Dhana kuhusiana na nyaraka za miaka thelathini.
106. Dhana kuhusiana na kumbukumbu za kielektroniki za miaka mitano.

SEHEMU YA KUMI NA TANO
UONDOAJI WA USHAHIDI WA MDOMO
KWA USHAHIDI WA HATI

107. Ushahidi wa masharti wa mikataba, utoaji na uhaulishaji mwengine wa mali kwa njia ya waraka.

108. Kuondolewa kwa ushahidi wa makubaliano ya mdomo.

109. Kuondoa ushahidi wa kuelezea au kurekebisha hati yenye utata.

110. Kuondoa ushahidi dhidi ya matumizi ya waraka kwa matukio yaliyopo.

111. Ushahidi kuhusiana na waraka usio na maana kuhusiana na matukio yaliopo.

112. Ushahidi kuhusiana na matumizi ya lugha ambayo ingeweza kutumika kwa mmoja tu kati ya watu kadhaa.

113. Ushahidi kuhusiana na matumizi ya lugha kwa kundi moja kati ya makundi mawili ya matukio, yasiyotumika kwa usahihi wa yeyote.

114. Ushahidi kuhusiana na maana ya tabia zisizoeleweka.

115. Nani anaeweza kutoa ushahidi wa makubaliano yanayopingana na masharti ya nyaraka.

116. Kubakishwa kwa masharti ya sheria ya mirathi kuhusiana na wasia.

SEHEMU YA KUMI NA SITA
JUKUMU LA KUTHIBITISHA

117. Jukumu la kuthibitisha.

118. Kwa nani dhima ya kuthibitisha inaangukia.

119. Dhima ya kuthibitisha tukio maalumu.

120. Dhima ya kuthibitisha tukio kuthibitishwa kufanya ushahidi ukubalike

121. Kiwango cha dhima ya kuthibitisha kuwa kwa mshitakiwa katika kesi Fulani.

122. Dhima ya kuthibitisha tukio hasa kwenye uelewa wa kesi za madai

123. Dhima ya kuthibitisha kifo cha mtu anaejulikana kuwa alikuwa hai ndani ya miaka thelathini.

124. Dhima ya kuthibitisha kwamba mtu yuko hai ambae hajasikika kwa miaka saba.

125. Dhima ya kuthibitisha uhusiano katika kesi ya wabia, mwenye ardhi au mpangaji, mtoa uwakala na wakala.

126. Dhima ya kuthibitisha umiliki.

127. Uthibitisho wa nia njema katika matendo pale ambapo upande mmoja katika mahusiano ya kujiamini.

128. Kizazi wakati wa ndoa ni uthibitisho tosha wa uhalali
129. Mahakama inaweza kuchukulia uwepo wa matukio fulani.

SEHEMU YA KUMI NA SABA
ZUIO

130. Zuio.
131. Mazuio kwa mpangaji, mtu aliyeruhusiwa au mtu aliyekalia.
132. Mazuio ya mpokea stakabadhi ya malipo, mdhaminiwa au mwenye kuruhusiwa.

SEHEMU YA KUMI NA NANE
MASHAHIDI

133. Nani anaweza kutoa ushahidi.
134. Mashahidi walio katika mazingira hatarishi na waliofanyiwa vitisho wanastahiki njia maalum.
135. Shahidi bubu au kiziwi.
136. Wadaawa katika kesi ya madai na wake zao au waume zao.
137. Jaji na Mahakimu.
138. Mawasiliano wakati wa ndoa.
139. Ushahidi unaohusu masuala ya Dola.
140. Afisa kuhusiana na masuala ya Dola.
141. Taarifa zinazohusiana na utendaji wa makosa.
142. Mawasiliano ya kitaalamu.
143. Kifungu cha 143 kutumika kwa wakalimani, n.k.
144. Upendeleo hauondolewi kwa kujitolea kutoa ushahidi.
145. Mawasiliano ya siri na washauri wa kisheria.
146. Kutoa waraka wa shahidi ambae si mdaawa.
147. Utoaji wa nyaraka au kumbukumbu za kielektroniki ambao mwengine mwenye kuzishikilia angekataa kuzitoa.
148. Shahidi hasameheki kujibu kwa msingi kwamba jibu litamfanya kuwa na hatia.
149. Mshiriki wa kosa.
150. Idadi ya mashahidi.

SEHEMU YA KUMI NA TISA
MAHOJIANO NA MASHAHIDI

151. Utaratibu wa kuwaita na kuwahoji mashahidi.

152. Mahakama kuamua kuhusu kukubalika kwa ushahidi.

153. Mahojiano makuu, mahojiano kinzani na mahojiano rejea.

154. Utaratibu wa mahojiano na maelekezo ya mahojiano rejea.

155. Mahojiano kinzani ya mtu aliyeitwa kutoa waraka.

156. Shahidi kuhusiana na tabia.

157. Maswali ya kuongoza.

158. Wakati gani maswali ya kuongoza hayataulizwa.

159. Wakati gani maswali ya kuongoza yanaweza kuulizwa.

160. Ushahidi kuhusiana na mambo yaliyo katika maandishi.

161. Mahojiano kinzani kuhusiana na maelezo ya maandishi yaliyopita.

162. Maswali halali katika mahojiano kinzani.

163. Wakati shahidi atalazimishwa kujibu.

164. Mahakama kuamua wakati gani swali litaulizwa na wakati gani shahidi atalazimika kulijibu.

165. Swali kutokuulizwa bila ya sababu ya msingi.

166. Utaratibu wa Mahakama iwapo swali limeulizwa bila ya sababu za msingi.

167. Maswali ya kuvunja heshima na yanayokashifu.

168. Maswali yaliyokusudiwa kutusi au kuudhi.

169. Uondoaji wa ushahidi hupinga majibu kwa maswali yanayothibitisha ukweli.

170. Swali kwa mdaawa kwa shahidi wake mwenyewe.

171. Kukanusha ukweli wa shahidi.

172. Maswali yanayohitaji kuungwa mkono na ushahidi wa matukio husika yanakubalika.

173. Maelezo ya nyuma ya shahidi yanaweza kuthibitishwa kuunga mkono ushahidi wa baadae kama tukio lile lile.

174. Mambo gani yanayoweza kuthibitishwa kuhusiana na taarifa husika zilizothibitishwa chini ya Kifungu cha 32 au 36.

175. Kujikumbusha na wakati shahidi anaweza kutumia nakla ya waraka kujikumbusha.

176. Ushahidi kwa matukio yaliyotajwa katika waraka iliyotajwa katika Kifungu cha 175.

177. Haki ya upande kinzani kuhusiana na maandishi yaliyotumika kujikumbushia.

178. Kutolewa kwa nyaraka na tafsiri ya nyaraka.

179. Kutoa, kama ushahidi wa waraka ulioitwa kwa, na kutolewa kwa notisi.

180. Kutumia, kama ushahidi, wa utoaji waraka ambao ulikataliwa kwa notisi.

181. Uwezo wa Mahkama kuuliza maswali au amri ya utowaji.

182. Uwezo wa washauri wa Mahakama kuuliza maswali.

SEHEMU YA ISHIRINI

KUKUBALI KUSIKO SAHIHI NA KUKATALIWA USHAHIDI

183. Hakuna kusikilizwa upya kwa kukubaliwa kusiko sahihi au kukataliwa ushahidi.

184. Uwezo wa kutunga kanuni.

185. Kufuta na kuhifadhi.

SHERIA NAMBA 9 YA 2016

NIMESAINI

Alhemin

{DK. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

18th January, 2017

SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA USHAHIDI SURA YA TANO NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA USHAHIDI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
VIFUNGU VYA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ushahidi, 2016 na itaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Rais.

Kutumika.

2. Isipokuwa kama itakavyoelezwa vyenginevyo katika Sheria nyengine yoyote, Sheria hii itatumika katika mienendo yote ya Mahakama au mbele ya Mahakama yoyote, lakini haitotumika kwa viapo vilivyowasilishwa mbele ya Mahakama au Afisa yeyote na wala haitotumika kwa mienendo mbele ya mtatuzi wa migogoro.

Tafsiri.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"**Afisa wa polisi**" maana yake ni mtumishi yeyote wa jeshi la polisi mwenye cheo cha chini au zaidi;

"**Inaweza kuchukuliwa**" maana yake ni iwapo itaelezwa na Sheria hii kwamba Mahakama inaweza kuchukulia tukio, inaweza ama kuchukulia kwamba tukio hilo limethibitishwa, isipokuwa na mpaka litakanushwa, au linaweza kuletwa kwa ajili ya kuthibitishwa;

"**Italazimika kuchukulia**" maana yake iwapo itaelekezwa na Sheria hii kwamba mahakama itachukulia tukio, italazimika kulichukulia tukio hilo kama limethibitika, isipokuwa na mpaka imekanushwa au inaweza kuleta kwa kulithibitisha;

"Kompyuta" maana yake ni chombo cha kielektroniki cha maginetiki, cha kuonesha au chombo chengine chenye kasi kubwa katika kufanyia kazi takwimu (data) au mfumo ambao unafanya kazi kimantiki, kihesabu, na kazi za kuhifadhi kumbukumbu kwa udhibiti wa kielectroniki, kimaginetiki, au msukumo wa hiari na utajumuisha uingiaji, utoaji, ufanyaji kazi, uhifadhi, program zote zilizo katika mfumo wa kompyuta au huduma za mawasiliano ambazo zimeunganishwa au zinahusiana na kompyuta katika mfumo wa kompyuta au mtandao wa kompyuta;

"Kuhusiana" maana yake ni tukio moja kuchukuliwa kwamba linahusiana na jengine pale ambapo yakiunganishwa pamoja kwa njia yoyote iliyotajwa katika masharti ya Sheria hii, yanatokana na matukio husika;

"Kumbukumbu za kielektroniki" maana yake ni kumbukumbu zilizotengenezwa, zilizotokana, zilizotumwa, zilizowasilishwa, zilizopokelewa, au kuhifadhiwa katika mfumo wa kielektroniki;

"Mahakama" inajumuisha Majaji, Mahakimu, na watu wote, isipokuwa watatuzi wa migogoro walioidhinishwa kisheria kuchukua ushahidi;

"Mambo yanayobishaniwa" ina maana ya:

(a) tukio lolote ambalo, ama lenyewe au kwa kuunganisha na matukio mengine kuwepo, kutokuwepo kwake, kimaumbile au kiwango cha haki yoyote, kuwajibika au kutowajibika, kukubalika au kutokubalika katika shauri au mwenendo ambao utalazimika kufuata;

(b) wakati wowote, chini ya masharti ya sheria inayotumika kuhusiana na mwenendo wa mashauri ya madai, kumbukumbu zozote za Mahakama tukio linalobishaniwa, tukio linalokubaliwa au kukanushwa katika majibu ya suala hilo ni suala linalobishaniwa;

"Mume au mke" maana yake ni wana ndoa halali kwa mujibu wa sheria ya kiislamu au sheria nyengine yoyote ya ndani au nje ya Zanzibar inayotambuliwa na mamlaka yenye uwezo;

"Mtaalamu" maana yake ni mtu mwenye uweledi na ujuzi wa kuthibitisha kisayansi, kiufundi, kitaaluma au jambo lolote mahsusi kwa sababu ya utambuzi wake juu ya jambo hilo au kutokana na ujuzi maalumu aliyoupata katika jambo hilo;

"Mkalimali" maana yake ni mtu ambaye atakula kiapo wakati wa kusikiliza kesi kwa lengo la kutafsiri kwa usahihi ushahidi wa mtu ambaye ni kiziwi au anazungumza lugha ya kigeni;

"Ndoa" maana yeke ni makubaliano ya hiyari baina ya mwanamke na mwanamume ambayo yatapelekea mwanamke kuitwa mke na mwanamume kuitwa mume yaliyofungwa kwa mujibu wa Sheria za dini, au sheria nyengine yoyote inayotumika ndani au nje ya Zanzibar;

"tukio hudaiwa kuthibitishwa" pale ambapo, baada ya kuzingatia jambo lililo mbele yake, Mahakama ama itaamini uwepo wake, au inazingatia uwezekano wa kutokea kwake kwamba mtu wa kawaida, katika mazingira ya hali husika, anapaswa kuchukulia kuwepo kwa jambo hilo;

"Tukio hudaiwa kutokuthibitishwa" pale ambapo, baada ya kuzingatia mambo yaliopo mbele yake, Mahakama ama inaamini kutokuwepo kwake au inazingatia uwezekano wa kutokuwepo kwake kwamba mtu wa kawaida katika mazingira ya kesi maalum atapaswa kuchukulia kwamba jambo hilo halikuwepo;

"Tukio linadaiwa kutothibitishwa" pale ambapo, jambo hilo halikuthibitishwa wala halikukanushwa;

"tukio" ina maana na inajumuisha:

(a) jambo lolote, hali za vitu, au uhusiano wa vitu vinavyoweza kuhisiwa kwa viungo vya ufahamu;

(b) hali yoyote ya kiakili ambayo mtu yeyote anafahamu;

"Ushahidi wa maneno" maana yake ni maelezo yote ambayo Mahakama inaruhusu au inahitaji yatolewe mbele yake na mashahidi, wakiwepo wakati wa kutoa maelezo au kwa kutumia njia nyengine za mawasiliano zikijumuisha mawasiliano ya mkutano kwa njia ya simu, mawasiliano ya mkutano kwa njia ya video yanayohusiana na matukio yanayochunguzwa;

"Ushahidi wa waraka" maana yake ni nyaraka zote zikiwemo kumbukumbu za kielektroniki zilizotolewa kwa ajili ya ukaguzi wa Mahakama;

"Ushahidi" inamaanisha njia ambayo jambo linalodaiwa kutokea, ukweli ambao ikiwa kama utawasilishwa kwa upelelezi, unaothibitisha au kukanushwa na bila kuathiri mwenendo kwa ujumla, unaojumuisha maelezo na kukiri kwa mshtakiwa;

"Uthibitisho usiopingika" maana yake iwapo tukio moja linatajwa nasheria hii kwamba ni uthibitisho usiopingika wa jambo jengine, Mahkama italazimika baada ya kuthibitisha jambo moja kulizingatia jengine kama limethibitika na haitaruhusu kutolewa ushahidi wa kukanusha ukweli uliothibitishwa;

"waraka wa kielektroniki" maana yake ni ujumbe, zana, taarifa, takwimu, picha, maandishi, programu, programu za Kompyuta, mfumo wa kitakwimu, au kitu kinachofanana, bila kujali jinsi gani kimetengezwa, ikiwa kitu hicho kinaweza kurudishwa au kuoneshwa katika hali ya kushikika;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya Sheria.

SEHEMU YA PILI
UHUSIANO WA MATUKIO

Ushahidi unaoweza ukatolewa kwa matukio yanayobishaniwa na matukio yanayohusiana.

4.(1) Ushahidi unaweza ukatolewa katika shauri lolote au mwenendo wa kuwepo au kutokuwepo kwa tukio linalobishaniwa na matukio mengineyo kama ambavyo yametajwa hapa kuwa ni yenye kuhusika, na si mengineyo.

(2) Kifungu hiki hakitomuwezesha mtu yeyote kutoa ushahidi wa tukio ambalo hapaswi kulithibitisha kwa mujibu wa masharti ya sheria inayotumika kuhusiana na mwenendo wa madai.

Uhusiano wa matukio yanayofanya sehemu ya tukio lile lile.

5. Matukio ambayo, ingawa si katika jambo linalobishaniwa yameungana na tukio linalobishaniwa na kufanya sehemu ya tukio lile lile, yanahusiana, kama yamefanyika kwa wakati huo huo au pahala hapo hapo au nyakati tofauti na mahala tofauti.

Matukio ambayokutokea kwake, sababu au athari za matukio yanayobishaniwa.

6. Matukio ambayo kutokea kwake, sababu au athari, punde au vyenginevyo,ya matukio yanayohusiana au matukio yanayobishaniwa au yanayofanya hali ya mambo ambayo yametokea, au yaliyotolewa fursa ya kutokea kwake au matendo, yanahusika.

Dhamira, maandalizi na hisia za kabla au baada.

7.(1) Tukio lolote linalohusiana ambalo linaonesha au kupelekea dhamira au maandalizi kwa tukio lolote linalobishaniwa au tukio linalohusika.

(2) Hisia ya mdaawa yeyote au wakala wa mdaawa yeyote, katika shauri au mwenendo wowote, linalohusiana na shauri au mwenendo huo au kuhusiana na tukio lolote linalobishaniwa au linalohusiana nalo, na hisia ya mtu yeyote, ambaye kosa dhidi yake linahusina na mwenendo wowote wa kesi, inahusika, iwapo hisia hiyo imeshawishi au imeshawishiwa na tukio lolote linalobishaniwa au linalo husika na iwapo lilikuwa kabla au baada ya hisia hiyo.

(3) Neno hisia katika kifungu hiki hakijumuishi maelezo, isipokuwa kama maelezo hayo yameambatana na kuelezea matendo yasiyokuwa maelezo, lakini ufafanuzi huu hautoathiri kuhusika kwa maelezo chini ya kifungu chochote cha Sheria hii.

(4) Ikiwa hisia ya mtu yoyote inahusiana, maelezo yoyote yaliyofanywa kwake au mbele yake na kusikia, ambayo inaathiri hisia hiyo basi inahusika.

Matukio ambayo ni muhimu kueleza au kutambulisha matukio husika.

8. Matukio ambayo ni muhimu kueleza au kutambulisha tukio linalobishaniwa au tukio linalohusika, au ambalo linathibitisha au kukanusha dhana iloletwa na tukio linalobishaniwa au tukio linalohusika, au ambalo linaoonesha utambulisho wa kitu chochote au mtu ambae utambulisho wake unahusika, au kuweka muda au mahala ambapo tukio lolote linalobishaniwa au tukio husika limetokea, au ambalo linaonesha mahusiano na wadaawa kwa ambae tukio hilo lolote lilifanywa, yanahusiana ilimradi ni muhimu kwa madhumuni hayo.

Vitu vilivyosemwa au kufanywa na mlanjama wakiwa na dhamira moja.

9. Pale ambapo kuna sababu za msingi za kuamini kwamba watu wawili au zaidi wamekula njama pamoja na kufanya kosa au tendo ovu, jambo lolote lililosemwa au kufanywa au kuandikwa na mmoja yeyote miongoni mwa watu hao kuhusiana na dhamira yao ya pamoja, baada ya muda ambao dhamira hiyo ilifanyika kwa mara ya mwanzo na yeyote miongoni mwao ni tukio husika dhidi ya kila mtu anayeaminiwa kula njama hiyo, kwa madhumuni ya kuthibitisha kuwepo kwa kula njama huko ili kuonesha kwamba yeyote miongoni mwao alikuwa sehemu ya njama hiyo.

Wakati ambao matukio hayahusiani vyenginevyo huwa yanahusika.

10. Wakati ambao matukio hayahusiani vyenginevyo huwa yanahusika:

(a) ikiwa kuna utofauti na hoja yoyote inayobishaniwa au tukio linalohusiana;

(b) ikiwa matukio hayo au kwa kuunganisha na matukio mengine yanafanya kuwepo au kutokuwepo kwa hoja yoyote inayobishaniwa au tukio linalohusiana kuwezekana au kutokuwezekana kwa kiasi kikubwa.

Katika mashauri yanayohusiana na fidia hoja zitakazoiwezesha Mahakama kutoa maamuzi ya kiwango zinahusika.

11. Katika mashauri ambayo yanayohusiana na malalamiko ya fidia, hoja yoyote ambayo itaiwezesha Mahakama kuamua kiwango cha fidia kilichotakiwa kulipwa, inahusika.

Hoja zinazohusika pale ambapo haki au desturi zinajadiliwa.

12. Pale ambapo mjadala unaohusiana na uwepo wa haki au desturi yoyote, hoja zifuatazo zinahusika:

(a) pale ambapo tendo lolote linalohusiana na haki au desturi inayojadiliwa lilifanywa, lililalamikiwa, lilirekebishwa, lilitambuliwa, lilikubaliwa, lilikataliwa au ambalo lilikinzana na kuwepo kwake; na

(b) matukio maalum ambayo haki au desturi iliyolalamikiwa, iliyotambulika au uliotekelezwa, au utekelezwaji wake ulikuwa ukibishaniwa ulikubaliwa au ulitafautiana

Matukio yanayoonesha uwepo wa hali ya ufahamu wa kiakili au kimwili au hisia za kimwili.

13.-(1) Matukio yanayoonesha ufahamu wowote wa kiakili kama nia, uelewa, nia njema, uzembe, uharaka, uwovu au wema kwa mtu yeyote au zinazoonesha uwepo wa hali ya kiakili, hali ya kimwili au hisia za kimwili, zinahusika, pale ambapo uwepo wa hali yoyote ya kiakili au kimwili au hisia za kimwili inajadiliwa au inahusika.

(2) Tukio husika linaloonesha uwepo wa hali halisi ya kiakili, lazima lioneshe kwamba uwepo wa hali ya kiakili, sio kwa ujumla, ila itahusisha mambo maalum yanayobishaniwa.

(3) Pale ambapo shtaka la mshitakiwa wa kosa la jinai, makosa ya mshitakiwa yaliyopita yatakuwa yanahusika kwa tafsiri ya kifungu hiki, hatia za makosa yake ya nyuma pia zitakuwa ni hoja zinazohusika.

Hoja zinazojadiliwa ama tendo limefanyika kwa bahati mbaya au kwa kukusudia.

14. Pale ambapo kuna mjadala ama tendo limefanyika kwa bahati mbaya au kwa kukusudia, au limefanyika kwa uelewa au kwa nia, hoja kwamba kitendo hicho kinaunda mlolongo wa matukio yaliyofanana, ambapo mtu aliyefanya tendo hilo lilimuhusu, inahusika.

Kuwepo kwa sababu za kutendeka kwa jambo ambalo linahusika.

15. Endapo kutakuwa na tendo fulani limefanywa, uwepo wa sababu yoyote ya kutendeka kwa jambo hilo lingefanyika kikawaida, ni hoja inayohusika.

SEHEMU YA TATU
KUKUBALI

Maana ya kukubali.

16. Kukubali maana yake ni, maelezo ya mdomo au maandishi au yaliyomo katika mfumo wa kieletroniki, ambayo yanatoa muelekeo katika hoja inayobishaniwa au hoja inayohusika, na ambayo imefanywa na watu wa aina yeyote, na katika mazingira yaliyotajwa.

Kukubali kwa mdaawa katika kesi au wakala wake au upande wenye maslahi.

17.(1) Maelezo yaliyosemwa na mdaawa katika kesi, au wakala wa mdaawa yeyote, ambae Mahakama inamtambua, katika mazingira ya kesi, ameruhusiwa na mdaawa kutoa maelezo kwa kauli au vitendo, ni kukubali.

(2) Maelezo yaliyofanywa na wadaawa katika madai ya kudai au kudaiwa katika hali ya kuwakilishwa, si kukubali, isipokuwa maelezo hayo yametolewa wakati mdaawa aliyeyatoa maelezo hayo alikuwa na sifa hiyo.

(3) Maelezo yaliyotolewa na:

(a) watu wenye umiliki au maslahi ya kifedha katika kiini cha kesi, na anaetoa maelezo katika sifa za watu wenye maslahi; au

(b) watu ambao miongoni mwa wadaawa katika dai wameonesha maslahi katika kiini cha dai;

ni kukubali, ikiwa yametolewa wakati wa muendelezo wa maslahi ya watu waliotoa maelezo hayo.

Kukubali kwa watu ambao nafasi zao lazima zithibitishwe dhidi ya mdaawa katika dai.

18. Maelezo yaliyotolewa na watu ambao nafasi zao au majukumu yao ni muhimu kuthibitisha dhidi ya mdaawa yeye katika dai, ni kukubali, kama maelezo hayo yatakuwa yenye kuhusiana dhidi ya watu hao kuhusiana na nafasi zao au dhima katika dai walilolifungua au lililofunguliwa dhidi yao, na ikiwa limefanywa wakati watu waliofanya walikuwa wamehodhi nafasi hii au wanawajibika kufanya dhima hiyo.

Kukubali kwa watu ambao moja kwa moja wametajwa na mdaawa katika dai.

19. Maelezo yaliyotolewa na watu ambao mdaawa katika dai aliowaorodhesha kwa maelezo ya kuhusiana na jambo linalobishaniwa ni kukubali.

Uthibitisho wa kukubali dhidi ya watu waliotoa maelezo hayo ya kukubali na au kwa niaba yao.

20. Kukubali kunahusiana na kunaweza kuthibitisha dhidi ya mtu aliyoyatoa, au muakilishi wake katika maslahi; lakini hakuwezi kuthibitishwa nae au kwa niaba ya mtu ambae anaeyatoa au kwa muakilishi wake katika maslahi, isipokuwa katika hali zifuatazo:

(a) kukubali kunaweza kuthibitishwa na mtu aliyeyatoa maelezo hayo au kwa niaba ikiwa katika hali ambayo, ikiwa watu walioyatoa wamefariki itakuwa inahusiana baina ya watu watatu katika kifungu cha 32 cha Sheria hii;

(b) kukubali kunaweza kuthibitishwa na mtu aliyeyatoa maelezo hayo au kwa niaba ikiwa itajumuisha na maelezo ya uwepo wa hali yoyote ya kiakili au kimwili, yanahusika au kubishaniwa, imefanywa au katika wakati ambao hali ya kiakili au kimwili ilikuwepo, na iliambatana na tendo lililopelekea uovu wake;

(c) Kukubali kunaweza kuthibitishwa na mtu aliyeyatoa maelezo hayo au kwa niaba ikiwa inahusiana vyenginevyo kuliko kukubali.

Wakati ambao kukubali kwa mdomo juu ya yaliyomo katika nyaraka ni yenye kukubalika.

21. Kukubali kwa mdomo dhidi ya yaliyomo katika nyaraka hakutakuwa na mahusiano, isipokuwa na mpaka mdaawa aliyependekeza kuthibitisha nyaraka hizo lazima aonyeshe anaweza kutoa ushahidi wa nakala ya nyaraka yale yaliyomo katika nyaraka husika kulingana na masharti yaliyomo katika Sheria hii, au isipokuwa uhalisia wa ile nyaraka ina mashaka.

Wakati ambao kukubali kwa mdomo kwa yaliyomo katika kumbukumbu za kielektroniki kunakubalika.

22. Kukubali kwa mdomo kwa yaliyomo ndani ya kumbukumbu za kielektroniki, haitahusika, isipokuwa uhalisia wa kumbukumbu ya kielektroniki iliyotolewa ina mashaka.

Ni wakati gani kukubali katika kesi za madai kunakubalika.

23.(1) Katika kesi za madai hakuna kukubali kunakohusika ikiwa kumefanywa ama kwa masharti ya maelezo kwamba ushahidi wake usitolewe, au katika mazingira ambayo Mahakama itachukulia kwamba wadaawa wamekubaliana kwamba ushahidi huo usitolewe.

(2) Hamna kitu chochote katika kifungu hiki kitakachotumika kumtoa wakili yeyote kutoa ushahidi wa jambo lolote ambalo anaweza kulazimishwa kutoa ushahidi huo chini ya kifungu cha 143 cha Sheria hii.

Kukubali sio uthibitisho kamili lakini kunaweza kuzuia.

24. Kukubali sio uthibitisho kamili kwa jambo lililokubaliwa, lakini kunaweza kutumika kama zuio chini ya masharti yaliyomo katika Sheria hii.

SEHEMU YA NNE
MAUNGAMO

Ni wakati gani ungamo lililosababishwa na ushawishi, kitisho au ahadi, haihusiani katika mwenendo wa jinai.

25. Ungamo lililofanywa na mshtakiwa halihusiki katika mwenendo wa kesi za jinai:

(a) ikiwa mfanyaji wa ungamo ameonekana na Mahakama kuwa ameshawishiwa, ametishiwa au ameahidiwa akiwa anahusishwa na shitaka dhidi ya mshtakiwa, kesi kutoka kwa mtu mwenye mamlaka; na

(b) kwa mtazamo wa Mahakama ushawishi huo, vitisho au ahadi unatosha kumpa mshtakiwa sababu zitakazoonekana ni za msingi kwa mdaiwa kwa kuonesha kwamba kwa kuungama angefaidika au angeepuka uovu wowote ambao ungemhusisha katika kesi dhidi yake.

Ungamo mbele ya Hakimu.

26. Ungamo lililofanywa na mtuhumiwa akiwa huru na kwa hiyari mbele ya hakimu linaweza kuthibitika dhidi yake.

Ungamo la mshtakiwa akiwa katika udhibiti wa Polisi halitathibitika dhidi yake.

27. Hakuna ungamo lililofanywa na mtu yeyote akiwa katika udhibiti wa Afisa wa Polisi, isipokuwa limefanywa mbele ya Hakimu, litathibitika dhidi yake.

Kiasi cha taarifa ambazo zimepokelewa kutoka kwa mshtakiwa zinaweza kuthibitishwa.

28. Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 27 cha Sheria hii, ikiwa jambo lolote lililotolewa kama lilivyoibuliwa katika mtiririko wa taarifa zilizopokelewa kutoka kwa mshtakiwa, katika udhibiti wa Afisa wa Polisi, kwa vile taarifa hizo zikiwa ni kuungama au kutokuungama, kama zinauhusiano wa karibu na mambo yaliyoibuliwa, linaweza kuthibitishwa.

Ungamo lililofanywa baada ya kuondolewa hisia zilizosababishwa na ushawishi, kitisho au ahadi, zinahusiana.

29. Ikiwa ungamo kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25 cha Sheria hii, limefanywa baada ya hisia zilizosababishwa na ushawishi, kitisho au ahadi, kwa maoni ya Mahakama, wote umeondolewa kuwa unafaa.

Ungamo ambalo vyenginevyo lisingehusika kwa sababu ya ahadi ya usiri.

30. Ikiwa ungamo vyenginevyo linahusika, haliwezi kuwa halihusiki kwa sababu tu limefanywa kwa ahadi ya usiri, au kufuati au danganyifu aliofanyiwa mshtakiwa kwa madhumuni ya kupatikana ungamo hilo, au wakati alikuwa amelewa, au ungamo limefanywa kwa majibu ya maswali ambayo hakutakiwa kuyajibu, kwa namna yoyote yatakavyokuwa maswali hayo, au kwa sababu hakutahadharishwa kwamba hakulazimika kufanya ungamo hilo, na kwamba ushahidi wake ungeweza kutolewa dhidi yake.

Zingatio la ungamo lililothibitika linamuathiri mtu aliyeungama na watu aliounganishwa nao katika kesi kwa kosa moja.

31.(1) Wakati watu zaidi ya mmoja watakaposhitakiwa pamoja kwa kosa lile lile, na ungamo lililofanywa na mmoja miongoni mwao linalomuathiri yeye na watu hao wengine inathibitika, Mahakama inaweza kuzingatia ungamo hilo dhidi ya watu hao wengine na pia dhidi ya mtu alieungama.

(2) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kutiwa hatiani kwa mshtakiwa hakutojikita moja kwa moja kwa ungamo lililofanywa na mshtakiwa mwenza.

(3) "Kosa" kama lilivyotumika katika kifungu hiki linajumuisha kusaidia, au kujaribu kufanya kosa.

SEHEMU YA TANO
MAELEZO YA WATU AMBAO HAWAWEZI KUITWA KAMA MASHAHIDI

Maelezo ya watu ambao hawawezi kuitwa kama mashahidi.

32. Maelezo, maandishi au maelezo ya mdomo, ya mambo yanahusika yaliyofanywa na mtu aliyefariki, au asieweza kupatikana, au asiyekuwa na uwezo wa kutoa ushahidi, au upatikanaji wake hauwezekani bila ya kuchelewa au kwa gharama ambayo katika mazingira ya kesi yanatokea mahakamani bila ya sababu, yenyewe ni mambo yenye kuhusika katika hali zifuatazo:

(a) endapo maelezo yametolewa na mtu wakati wa kifo chake, au kwa mazingira yoyote ya mtiririko uliosababisha kifo chake katika kesi ambazo sababu za kifo cha mtu huyo inajadiliwa, maelezo hayo yanahusika ikiwa mtu ambae ametoa maelezo hayo alikuwepo au hakuwepo wakati wa kutoa maelezo, anapokaribia kifo, na inawezekana maumbile ya mwenendo uliosababababisha kifo chake yanajadiliwa;

(b) wakati maelezo yametolewa na mtu katika shughuli zake za kawaida, na hasa inapotokana na ingizo lolote au makubaliano aliyoyafanya katika madaftari, au za kielektroniki, zilizowekwa katika shughuli za kawaida, au katika kutekeleza majukumu ya utaalam, au kutambua maandishi au saini yake katika risiti ya pesa, bidhaa, dhamana au mali ya aina yoyote au kumbukumbu za waraka uliotumika katika biashara zilizoandikwa au kusainiwa na yeye, au tarehe ya barua au waraka mwengine ambao kwa kawaida huwekwa tarehe, kuandikwa au kusainiwa na yeye;

(c) wakati maelezo yanapingana na maslahi ya kifedha au kimali ya mtu aliyeyatoa, au wakati, ikiwa ni kweli, ingemletea au ingeweza ingemdhihirisha katika mashtaka ya jinai au dai la madhara;

(d) wakati maelezo yanatoa maoni ya mtu yeyote, kwa kuwepo haki yoyote ya umma au mila au jambo ambalo ni la umma au maslahi ya jumla, ambayo kuwepo kwake, kama yalikuwepo, angeweza kuwa mwenye kujua, na pale ambapo maelezo hayo yamefanya mbele ya kupingana kokote na haki hiyo, mila au jambo lililojitokeza;

(e) wakati maelezo yanahusu kuwepo uhusiano wa damu, ndoa au kuasili baina ya watu ambao uhusiano wa damu, ndoa au kuasili, mtu anaetoa maelezo ana njia maalum ya kufahamu, na wakati maelezo yamefanywa kabla ya suala linalobishaniwa kuzuka;

(f) wakati maelezo yanahusiana na kuwepo kwa mahusiano yoyote ya damu, ndoa au kuasili baina ya watu ambao ni marehemu, na yametolewa katika wasia au hati inayohusiana na maswala ya kifamilia ambayo marehemu

alitokana nayo, au katika uasili wowote wa familia au jiwe lolote la kaburi, utambulisho wa familia au kitu chengine ambacho maelezo kama haya hufanywa, na wakati maelezo hayo yanafanywa kabla ya suala linalobishaniwa kuibuka;

(g) wakati maelezo yaliyomo katika hati yoyote, wasia au wakara mwengineo unaohusiana na jambo lolote kama ilivyotajwa katika aya (a) ya kifungu cha 12 cha Sheria hii; au

(h) wakati maelezo yaliyotolewa na idadi ya watu, na kueleza hisia au mitazamo yao yanahusiana katika jambo linalobishaniwa.

Kukubalika kwa kumbukumbu za biashara.

33.-(1) Katika mwenendo wowote wa jinai ambapo ushahidi wa moja kwa moja wa mdomo wa tukio linalohusika ungelikubalika, maelezo yoyote yaliyomo katika maandishi yoyote kumbukumbu au waraka katika mfumo wowote wa ingizo lolote katika daftari au katika mfumo mwengine wowote na ambao unapelekea kuanzisha tukio hilo kwa kutoa maandishi hayo, kumbukumbu au waraka, kutakubalika kama ushahidi wa tukio hilo iwapo:

(a) maelezo yamefanywa kama makubaliano au kumbukumbu ya tendo, shughuli ya kibiashara, kutokea au tukio, au

(b) maandishi ya kumbukumbu au warakani, au inafanya sehemu ya, kumbukumbu zinazohusiana na biashara yoyote na ili au iliyofanywa au kukusanywa katika shughuli ya kawaida ya kibiashara ambapo ni kawaida kuweka kumbukumbu ya tendo hilo, shughuli za kibiashara, kutokea au tukio linapotokea au ndani ya muda muafaka.

(2) Mazingira mengine yoyote yakutoa maelezo, ikijumuisha ukosefu wa uelewa wa mtu aliyetoa maelezo hayo inaweza kuchukuliwa kama inaathiri uzito wake kama ni ushahidi lakini hali zote hizo hazitoathiri kukubalika kwake.

(3) Katika kutathimini uzito wa kuunganishwa na maelezo ambayo yanakubalika kama ushahidi kwa mujibu wa kifungu hiki, zingatio litafanywa kwa mazingira yote ambayo hisia inaweza kuwepo kimsingi juu ya usahihi au vyenginevyo wa maelezo, na hasa kwa suala kama mtu anayetoa maelezo hayo, au anayehusiana na kuyafanya au kwa kuyahifadhi kwa maandishi, kurikodi au waraka ulio na melezo hayo, ana au hana motisha wa kuficha au upotoshaji wa matukio hayo.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "shughuli" inajumuisha shughuli, kazi, taaluma, biashara au itakavyoitwa vyovyote, "maelezo" inajumuisha uwasilishwaji wowote wa jambo, ikiwa limefanywa kwa maneno au katika njia nyengine yoyote.

Uthibitisho wa maelezo ya kimaandishi katika mwenendo wa jinai.

34.-(1) Katika mienendo yoyote ya jinai ambapo ushahidi wa moja kwa moja kwa njia ya mdomo juu ya ukweli unaohusika utakubalika, maelezo ya maandishi ya mtu yeyote ambaye ni, au anaweza, kuwa shahidi, kwa mujibu wa mashariti yafuatanyo ya kifungu hiki, yatakubalika katika ushahidi kama ni uthibitisho wa tukio husika uliomo ndani yake badala ya ushahidi wa moja kwa moja kwa njia ya mdomo.

(2) Maelezo ya maandishi yanaweza tu kukubalika chini ya kifungu hiki:

(a) pale ambapo mtoaji hakuitwa kama shahidi, kama atakuwa amefariki au hafai kwa sababu ya hali ya kimwili au kiakili hawezi kuhudhuria kama shahidi, au endapo yupo nje ya Tanzania na haiwezekani kuitwa kama shahidi, au endapo hatua zote zinazofaa zimechukuliwa kuwezesha kuhudhuria kwake lakini hawezi kupatikana au hawezi kuhudhuria kwa sababu hakuweza kutambulika au kwa mujibu wa sheria yoyote hawezi kuhudhuria;

(b) ikiwa maelezo yamesainiwa, au yanapaswa kusainiwa na mtu aliyeyatoa;

(c) ikiwa yana tamko la mtu aliyetoa tamko kwa kiasi kwamba ni kweli kwa kadri anavyofahamu na kuamini na ametoa maelezo akijua kwamba ikiwa yatatolewa katika ushahidi atakuwa atastahiki kushtakiwa kwa kutoa ushahidi wa uongo iwapo kwa ridhaa yake alieleza katika maelezo hayo jambo lolote ambalo alijua ni la uongo au hakuamini kuwa si la ukweli;

(d) ikiwa, kabla ya kusikilizwa kesi ambayo maelezo yanapaswa kutolewa kama ushahidi, nakala ya maelezo hayo itatumwa na au kwa niaba ya upande unaopendekeza kuyatoa, kwa kila mdaawa katika mwenendo huo;

(e) ikiwa, hakuna upande wowote, ndani ya siku kumi kuanzia tarehe ya kutumwa nakala ya maelezo, uliotuma notisi kwa upande unaopendekeza kutoa au kupinga kutolewa kwa maelezo hayo kama ushahidi;

(f) iwapo maelezo yamefanywa na mtu ambae hawezi kuyasoma, anasomewa kabla ya kuyasaini na yataambatanishwa na tamko la mtu aliyeyasoma kuonyesha kwamba amesomewa.

(3) Bila ya kujali kwamba maelezo ya maandishi yaliyotolewa na mtu yeyote yanaweza kukubalika kama ni ushahidi kwa madhumuni ya kifungu hiki:

(a) upande ambao, au kwa niaba yake nakla ya maelezo ilitumwa, anaweza kumwita mtu huyo kutoa ushahidi; na

(b) Mahakama yenyewe, au kwa maombi ya upande wowote katika mwenendo wa kesi, inaweza kumtaka mtu huyo kufika mbele ya Mahakama na kutoa ushahidi.

(4) Maelezo yote kama yalivyopokelewa kwa mujibu wa kifungu hiki, ispokuwa kama Mahakama itaelekeza vyenginevyo, yatasomwa kwa sauti wakati wa kusikiliza kesi na iwapo mahakama itaelekeza hivyo yatatolewa kwa mdomo kama hayakusomwa kwa sauti yatatolewa kwa mdomo kwa kiasi ambacho maelezo yoyote hayasomwi kwa sauti.

(5) Hati au kitu chochote kilichotolewa kama ni kielelezo na kimetajwa katika maelezo ya maandishi yaliyotolewa katika ushahidi chini ya kifungu hiki, kitazingatiwa kama kilitolewa kuwa kielelezo na kitatambuliwa Mahakamani na mtoa maelezo.

(6) Kwa madhumuni ya kanuni yoyote ya sheria au uzoefu unaohitaji kwamba ushahidi kuungwa mkono au kwamba ushahidi usioungwa mkono uchukuliwe kuwa ni maelezo yanayokubalika kwa mujibu wa kifungu hiki haitazingatiwa kuwa ni ushahidi wa kuungwa mkono uliotolewa na mtoaji maelezo hayo.

Uthibitisho wa maelezo ya maandishi katika mienendo ya madai.

35.-(1) Katika mwenendo wowote wa madai ambapo maelezo ya ushahidi wa moja kwa moja uliotolewa kwa mdomo wa tukio utakuwa unakubalika, maelezo yoyote yatakayofanywa na mtu katika hati yaliyokusudiwa kuonesha tukio hilo, katika utoaji wa hati halisi yatakubalika kuwa ni ushahidi wa jambo hilo pasi na kuwepo shahidi ikiwa hali zifuatazo zitafikiwa:

(a) ikiwa mtoaji maelezo aidha:

(i) alikuwa na uelewa wa mambo yaliyomo katika maelezo; au

(ii) ikiwa waraka husika ni sehemu au inafanya kuwa sehemu ya rikodi inayodaiwa kuwa ni rikodi endelevu, alitoa maelezo kwa mambo aliyoshughulikia yasiyo katika uelewa wake, katika kutekeleza wajibu wake wa kurikodi taarifa zilizoletwa kwake na mtu ambae anaufahamu, au kimsingi anapaswa kuwa na ufahamu wa mambo hayo; na

(b) ikiwa mtoaji wa maelezo ameitwa kama shahidi katika kesi, lakini sharti kwamba mtoaji wa maelezo ataitwa kama shahidi haitohitajika kuridhishwa ikiwa amefariki au hawezi kwa sababu ya hali yake ya kimwili au kiakili kuhudhuria kama shahidi au hayuko katika Tanzania na ni vigumu kupatikana, au ikiwa juhudi zote za kumtafuta, au za kumtambua, zimefanywa bila ya mafanikio.

(2) Katika mwenendo wowote wa kesi ya madai, Mahakama inaweza katika hatua yoyote ya kesi, baada ya kuzingatia mazingira yote ya kesi imejiridhisha kwamba ucheleweshwaji usio wa lazima au gharama ungeweza kusababisha kutoa amri kwamba maelezo yaliyotajwa katika kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki yatakubalika kama ushahidi au inaweza, bila ya kuwepo kwa amri iliyotolewa, itakubali maelezo yaliyotolewa katika ushahidi:

(a) bila ya kujali kwamba mtoa maelezo anapatikana lakini hakuitwa kama shahidi;

(b) bila ya kujali kwamba waraka halisi haukutolewa, ikiwa badala ya waraka halisi kumetolewa nakala ya waraka halisi au sehemu ya waraka huo umethibitishwa katika amri au kama Mahakama itakavyoidhinisha.

(3) Hakuna jambo lolote katika kifungu hiki litakalopelekea kukubalika kama ushahidi maelezo yoyote yaliyotolewa na mtu mwenye maslahi wakati kesi zilipokuwa zinasubiria au zinatarajiwa kuingiza mgogoro wa tukio lolote ambalo maelezo yangeweza kupelekea kuanzisha.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, maelezo katika waraka hayatochukuliwa kuwa yamefanywa na mtu isipokuwa waraka au sehemu ya waraka huo uliandikwa, ulifanywa au ulitolewa na yeye kwa mkono wake au ulitiwa saini au aliyeianzisha au vyenginevyo aliitambua kwa maandishi kama mmoja kwa usahihi ambao anawajibika nao.

(5) Kwa madhumuni ya kuamua maelezo yanakubalika au hayakubaliki kama ushahidi kwa mujibu wa kifungu hiki, Mahakama inaweza kupelekea kufanya hitimisho la msingi kutoka katika namna au maudhui yaliyomo katika waraka wenye maelezo, au kutoka katika mazingira yoyote, na inaweza katika kuamua mtu anafaa au hafai kuhudhuria kama shahidi, kutoa cheti kitakachoonesha kuwa ni cheti cha daktari aliyesajiliwa; na, bila ya kujali kwamba mahitaji ya kifungu hiki yametimizwa kuhusiana na maelezo, Mahakama kwa uwezo iliyonao inaweza kukataa maelezo ikiwa kwa sababu yoyote mahakama itakavyoona inafaa kwa ajili ya maslahi ya utekelezaji wa haki kwamba maelezo hayo yangekubalika.

(6) Katika kutathmini uzito, ikiwa upo, utakaoambatanishwa katika maelezo yaliyokubalika kama ushahidi kwa mujibu wa kifungu hiki, zingatio litawekwa kwa mazingira yote yanayoweza kupelekea kufanya hitimisho juu ya usahihi au vyenginevyo, na hasa juu ya suala la kwamba kama maelezo yalifanywa pamoja na kutokea kwa tukio lililotajwa, na juu ya suala la kwamba au la mtoa maelezo alikuwa na jambo lililompelekea kuficha maelezo.

(7) Kwa madhumuni ya kanuni yoyote ya sheria au uzoefu unaohitaji ushahidi wa kusaidia au kuweka utaratibu ambao ushahidi usioungwa mkono ungechukuliwa, maelezo yanayokubalika kama ushahidi kwa mujibu wa kifungu hiki hayatochukuliwa kama ushahidi wa kusaidia uliotolewa na mtoaji maelezo.

Uhusiano wa baadhi ya ushahidi kwa kuthibitisha kesi zilizotokea baada, ukweli wa matukio yaliyotajwa.

36.-(1) Ushahidi uliotolewa na shahidi katika mwenendo wa Mahakama, au mbele ya mtu yeyote aliyeidhinishwa na sheria kuchukua ushahidi huo, ni kwa mujibu wa masharti ya sheria nyengine yoyote inayotumika, inayoendana kwa dhumuni la kuthibitisha kesi ziliopo Mahakamani au katika hatua nyengine za kesi hiyo hiyo, ukweli wa matukio ambao unaeleza, endapo shahidi amefariki au hawezi kupatikana, au hawezi

kutoa ushahidi, au ameondolewa na upande kinzani, au hawezi kupatikana bila ya kuchelewa au gharama ambazo, kwa mazingira ya kesi, Mahakama inaona si ya msingi, isipokua kwamba:

(a) kesi ilikuwa ni baina ya wadaawa wale wale au wawakilishi wao kimaslahi;

(b) upande kinzani katika mwenendo wa awali wa kesi ulikuwa na haki na fursa ya kuuliza maswali; na

(c) masuala yanayobishaniwa kimsingi yalikuwa ni yale yale katika mwenendo wa mwanzo na wa pili.

(2) Mwenendo wa jinai au uchunguzi utachukuliwa kuwa ni mwenendo baina ya mwendesha mashtaka na mshtakiwa kwa maana ya kifungu hiki.

SEHEMU YA SITA
MAELEZO YALIYOFANYWA KWENYE MAZINGIRA MAALUM

Maingizo katika vitabu vya mahesabu yanapohusiana.

37. Maingizo katika vitabu vya hesabu yanajumuisha maingizo yote yaliyohifadhiwa katika mfumo wa kielektroniki, maingizo ya kawaida ya shughuli za kibiashara, yanahusiana wakati yatakapohusishwa na jambo ambalo Mahakama inalichunguza, lakini maelezo hayo pekee hayatokuwa ushahidi unaojitosheleza katika kumtia mtu yeyote hatiani.

Uhusiano wa ingizo katika kumbukumbu za umma zilizofanywa katika kutekeleza majukumu.

38. Ingizo katika vitabu nyengine vya umma au kitabu chengine rasmi, daftari la usajili, kumbukumbu au kumbukumbu za kielektroniki inayoeleza hoja bishaniwa au hoja husika, na iliyofanywa na mtumishi wa umma katika utekelezaji wa majukumu yake, au kwa mtu mwengine yeyote katika utekelezaji wa majukumu hasa yanayotambuliwa na sheria ya nchi ambapo daftari, daftari la usajili, kumbukumbu au kumbukumbu za kielektroniki zimehifadhiwa, yenyewe ni matukio yanayohusiana.

Uhusiano wa maelezo kwenye ramani, michoro na mipango.

39. Maelezo ya matukio yanayobishaniwa au yanayohusiana, yaliyomo katika ramani iliyochapishwa au michoro inayotolewa kwa ajili ya mauzo kwa umma, au katika ramani au mipango iliyofanywa chini ya mamlaka ya Serikali, kwa mambo ambayo kwa kawaida huwasilishwa au hutajwa katika ramani hizo, michoro au mipango hiyo ni mambo yanayohusiana.

Uhusiano wa maelezo juu ya matukio ya umma yaliyomo katika sheria fulani, gazeti au taarifa.

40. Endapo Mahakama inatoa maoni juu ya uwepo wa matukio yoyote ya umma, maelezo yoyote yaliyofanywa juu ya jambo hilo, kwa kumbukumbu iliyomo katika sheria yoyote inayotumika Zanzibar au katika taarifa ya Serikali iliyotolewa katika Gazeti Rasmi au katika chapisho lolote, litakalojulikana kuwa ni Gazeti Rasmi la Serikali ni tukio linalohusiana.

Uhusiano wa maelezo kwa sheria yoyote iliyomo katika vitabu vya sheria.

41. Endapo Mahakama inapaswa kutoa maoni kuhusiana na sheria ya nchi yoyote, maelezo yoyote ya sheria hiyo yaliyomo katika kitabu kinachodaiwa kunakiliwa au kuchapishwa chini ya mamlaka ya Serikali ya nchi hiyo na kuwa na sheria yoyote hiyo, na taarifa yoyote ya uamuzi wa Mahakama ya nchi hiyo iliyomo katika kitabu inayodaiwa kuwa ni taarifa ya uamuzi huo, inahusiana.

Ushahidi uliopatikana kwa njia ya siri.

42. Katika mienendo ya kesi zozote za jinai:

(a) taarifa zilizopatikana kutoka katika mfumo wa kompyuta, mitandao au mfumo wa kuhifadhia taarifa yatakubaliwa katika ushahidi;

(b) kumbukumbu zilizopatikana kupitia uchunguzi kwa njia za kulinda taarifa zinazojumuisha mashine ya barua pepe, uwasilishaji wa kielektroniki na miundombinu ya kimawasiliano yatakubaliwa katika ushahidi; au

(c) mfumo wa kurikodi matukio ya sauti au ya picha au tabia au mazungumzo ya watu walioshtakiwa, yatakubaliwa katika ushahidi

Namna ya maelezo yanayotakiwa kuthibitishwa.

43. Wakati maelezo yoyote ambayo yametolewa ushahidi yanafanya kuwa sehemu ya maelezo au mazungumzo au sehemu ya waraka pekee au imejumuisha au imo katika waraka ambao ni sehemu ya kitabu, au sehemu ya kumbukumbu za kielektroniki au zimo katika mtiririko wa herufi au nyaraka, ushahidi utatolewa na si zaidi ya maelezo, mazungumzo,waraka, kumbukumbu za kielectroniki, kitabu au msururu wa herufi au nyaraka au Mahakama itakavyoona inafaa katika kesi husika kwa uwelewa kamili wa asili na matokeo ya maelezo, na kwa mujibu wa mazingira jinsi ilivyofanyika.

SEHEMU YA SABA
HUKUMU ZA MAHAKAMA WAKATI ZINAPOHUSIKA

Hukumu zilizopita zinahusika katika kuzuia shauri la pili au kusikiliza.

44. Uwepo wa hukumu yoyote, amri au amri baada ya hukumu ambayo kwa mujibu wa sheria inazuia Mahakama yoyote kulitambua shauri au kuendesha kesi, ni tukio husika pale ambapo suala linalopaswa kuamuliwa ni kama Mahakama ilipaswa kuitambua kesi hiyo au kuendesha kesi hiyo.

Uhusiano wa hukumu fulani katika baadhi ya kesi za madai.

45.-(1) Hukumu ya mwisho, amri au amri baada ya hukumu ya Mahakama yenye uwezo, katika kutekeleza mamlaka ya kimirathi, masuala ya ndoa, masuala yanayohusiana na makosa ya bahari, au kufilisi, ambayo inaipa au kuchukua kutoka kwa mtu yeyote masuala yoyote ya kisheria au ambayo yanamtangaza mtu yeyote kupaswa kuwa na sifa yoyote ya kisheria, au kustahikiwa na jambo lolote maalumu isipokuwa kwa mtu mwengineo aliyeainishwa lakini bila ya masharti, inahusika pale ambapo kuwepo kwa sifa yoyote ya kisheria, au cheo cha mtu yeyote huyo kwa jambo lolote hilo linahusika.

(2) Hukumu hiyo, amri au amri baada ya hukumu ni uthibitisho kamili kwamba:

(a) sifa ya kisheria, pale ambapo inatokea wakati hukumu hiyo, amri au amri baada ya hukumu inapofanya kazi;

(b) sifa ya kisheria, ambayo inatamka mtu yeyote huyo kustahiki, kutimia kwa mtu huyo wakati hukumu hiyo, amri au amri baada ya hukumu inaitamkia kutimia kwa mtu huyo;

(c) sifa ya kisheria iliyoenguliwa kutoka kwa mtu yeyote inasita wakati ambao hukumu hiyo, amri au amri baada ya hukumu, inapotangaza kwamba ilisita au itapaswa kusita; na

(d) jambo lolote ambalo litaamua kwa mtu yeyote kuwa ni mmiliki wa mali ya mtu huyo pale ambapo hukumu hiyo, amri au amri baada ya hukumu, inaamua kwamba itakuwa au ingekuwa ni mali yake.

Uhusiano na athari za hukumu, amri, au amri baada ya hukumu, zisizokuwa zile ambazo zimetajwa katika kifungu cha 45.

46. Hukumu, amri au amri baada ya hukumu zisizokuwa zile ambazo zimetajwa katika kifungu cha 45 cha Sheia hii zinahusika ikiwa zitakuwa na mahusiano na masuala ya umma yanayohusiana na uchunguzi; lakini hukumu hizo, amri au amri baada ya hukumu hazitokuwa uthibitisho kamili kwa wanayoyaeleza.

Hukumu zisizokuwa zile zilizotajwa katika kifungu cha 44 na 45 namna zinavyohusika.

47. Hukumu, amri au amri baada ya hukumu zisizokuwa zile zilizotajwa katika vifungu vya 44 na 45 vya Sheria hii hazihusiki, isipokuwa uwepo wa hukumu hiyo, amri au amri baada ya hukumu ndio jambo linalobishaniwa au, linahusika kwa mujibu wa masharti mengineyo ya Sheria hii.

Udanganyifu, au kula njama katika kupatikana kwa hukumu.

48. Mdaawa yeyote katika shauri au mienendo mengine ya madai inaweza kuonesha kwamba hukumu yoyote, amri au amri baada ya hukumu ambazo zinahusika kwa mujibu wa vifungu vya 44, 45 au 46 vya Sheria hii na ambazo zimethibitishwa na upande kinzani, imetolewa na Mahakama ambayo haina uwezo wa kutoa maamuzi hayo au yamepatikana kwa njia ya udanganyifu au ulaji njama.

SEHEMU YA NANE
MAONI YA MTU WA TATU YANAPOHUSIKA

Maoni ya wataalamu.

49. Pale ambapo Mahakama inapaswa kutoa maoni kuhusiana na suala la sheria za kigeni au sayansi au sanaa au utambulisho wa maandishi au alama za vidole au umbo la dole gumba, maoni yanayotokana na hoja ya watu hao ni za ujuzi katika sheria za kigeni, sayansi, au sanaa au katika jambo kama ni utambulisho wa maandishi au kidole au umbile la kidole gumba ni hoja zinazohusika; watu hao wataitwa wataalamu.

Mambo yanayozingatiwa katika maoni ya wataalamu.

50. Mambo, yasiyohusiana vyenginevyo, yanahusiana ikiwa yanaunga mkono au yanakinzana na maoni ya wataalamu, wakati maoni hayo yanahusika.

Maoni ya maandishi ya mkono yanapohusika.

51.-(1) Wakati Mahakama itapaswa kutoa maoni kwa mtu ambae ameandika au kuzitia saini nyaraka zozote, maoni ya mtu yeyote yanayohusiana na maandishi ya mkono ya mtu ambae ilitakiwa iandikwe au isainiwe kwamba iliandikwa au haikuandikwa au kusainiwa na mtu huyo, ni jambo linalohusika.

(2) Mtu anadaiwa kuwa muelewa wa muandiko wa mtu mwengine endapo amemuona mtu huyo akiandika au amepokea hati zilizoandikwa na mtu huyo katika kujibu hati zilizoandikwa na mtu huyo katika shughuli za kawaida hati zinazodaiwa kuandikwa na mtu huyo zimekua na tabia za kuwasilishwa kwake.

Pale ambapo maoni yanayohusiana na uwekaji saini ya kidigitali yanapohusika.

52. Pale ambapo Mahakama inapaswa kutoa maoni yanayohusiana na saini ya kidigitali ya mtu yeyote, maoni ya Mamlaka inayothibitisha ambayo imetoa cheti cha saini ya kidigitali ni tukio linalohusika.

Maoni ya uwepo wa haki au desturi yanapohusika.

53.-(1) Pale ambapo Mahakama inapaswa kutoa maoni yanayohusiana na uwepo wa desturi au haki, maoni, ya uwepo wa desturi hiyo au haki, za watu ambao kuna uwezekano wa kujua uwepo wake ikiwa ilikuwepo yanahusika.

(2) Maneno "desturi au haki za jumla" inajumuisha desturi au haki zinazofuatwa na tabaka la watu.

Maoni yanayohusiana na matumizi ya imani yanapohusika.

54. Pale ambapo mahakama inapaswa kutoa maoni yanayohusiana na:

(a) matumizi na imani ya watu wowote au familia;

(b) uwanzishwaji na uongozi wa taasisi za kidini na jumuiya zozote za misaada; au

(c) maana ya maneno au misamiati iliyotumika katika Wilaya maalum au kwa tabaka la watu maalum,

maoni ya watu wenye elimu maalum ni matukio yanayohusika.

Maoni ya mahusiano yanapohusika.

55.-(1) Pale ambapo Mahakama itapaswa kutoa maoni juu ya uhusiano wa mtu mmoja kwa mwengine, maoni, yaliyoelezewa kwa hisia, juu ya uwepo wa uhusiano huo, kwa mtu yeyote ambae, akiwa ni mwanafamilia au vyenginevyo, ana uelewa maalum wa jambo hilo, ni tukio linalohusiana.

(2) Maoni chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hayatatosheleza kuthibitisha ndoa katika mashauri chini ya Sheria za ndoa au mashtaka kwa makosa ya zinaa au kuolewa na mume zaidi ya mmoja zinazoadhibiwa chini ya Sharia ya Adhabu.

Sababu za maoni zinapohusika.

56. Pale ambapo maoni ya mtu yeyote aliye hai yanahusika, sababu ambazo zimejikita katika maoni hayo nazo pia zinahusika.

SEHEMU YA TISA
WAKATI TABIA ZINAPOHUSIKA

Katika mashauri ya madai kuthibitisha hisia zilizoshutumiwa haihusiani.

57. Katika mashauri ya madai tukio kwamba tabia ya mtu yeyote anayehusika katika kupelekea kuwezekana au kutokuwezekana kwa hisia yoyote inayoshutumiwa kwake haihusiani, isipokuwa kama tabia hiyo inatokana na matukio ambayo vyenginevyo yanahusiana.

Katika kesi za jinai, tabia njema za wakati uliopita zinahusiana.

58. Katika mwenendo wa kesi za jinai tukio kwamba mshtakiwa ana tabia njema inahusiana.

Tabia mbaya za wakati uliopita hazihusiani, isipokuwa katika majibu.

59.-(1) Katika mwenendo wa kesi za jinai tukio kwamba mshtakiwa ana tabia mbaya haihusiani, isipokuwa kama ushahidi umetolewa kwamba ana tabia njema, na katika hali hiyo utakua unahusika.

(2) Kifungu hiki hakitumiki kwa mashauri ambayo tabia mbaya ya mtu yeyote yenyewe ni jambo linalobishaniwa.

(3) Kutiwa hatiani kwa makosa yaliyopita kunahusika kama ushahidi wa tabia mbaya.

Tabia zinazoathiri fidia

60.-(1) Katika kesi za madai suala ambalo tabia ya mtu yeyote ambayo kwa kiasi itaathiri kiwango cha fidia anachopaswa kupata, inahusika.

(2) Katika vifungu vya 57, 58, 59 na 60 vya Sheria hii neno "tabia" linajumuisha heshima na sifa; lakini isipokua kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 59 cha Sheria hii, ushahidi unaweza kutolewa kwa heshima ya jumla tu na sifa ya jumla, na sio kwa matendo maalumu ambayo heshima au sifa zimeonyeshwa.

SEHEMU YA KUMI
MATUKIO AMBAYO HAYAHITAJI KUTHIBITISHWA

Matukio yanayotambuliwa naMahakama hayahitaji kuthibitishwa.

61. Hakuna tukio ambalo Mahakama itachukulia kulitambua litakalothibitishwa.

Matukio ambayo yanapaswa kutambuliwa na mahakama.

62.-(1) Mahakama itachukulia utambuzi wa kimahakama juu ya matukio yafuatayo:

(a) Sheria zote zilizoandikwa, Taratibu, Kanuni, tamko la sharia, amri au notisi zenye nguvu za kisheria ndani ya Zanzibar;

(b) kuwepo na majina ya jumuiya au vyombo vyenginevyo ambavyo usajili wake umetangazwa katika Gazeti;

(c) kumbukumbu za mwenendo wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(d) kuwepo kwa ofisi, majina, cheo, kazi na sahihi za watu wanaoshikilia ofisi yoyote ya umma katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano, ikiwa tukio la uteuzi wao katika ofisi hiyo umetangazwa katika Gazeti;

(e) mihuri yote ya Mahakama zote ya sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania iliyoanzishwa kihalali na za wakuu wa viapo, na mihuri yote ambayo mtu yeyote ameidhinishwa kutumia na sheria yoyote.

(f) kuwepo, cheo, bendera ya Zanzibar na bendera ya Taifa ya kila Nchi au Mamlaka inayotambulikana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(g) mgawanyo wa muda, mgawanyo wa kijografia wa kiulimwengu, matamasha ya kitaifa, sikukuu na siku za mapumziko zilizotangazwa katika Gazeti Rasmi;

(h) kuanzishwa, kuendelezwa na kusitishwa kwa uhasama baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Nchi nyengine yoyote au chombo cha watu;

(i) majina ya wajumbe na maafisa wa Mahakama na ya manaibu wao na maafisa wasaidizi na wasaidizi, na maafisa wote wanaokaimu katika kutekeleza shughuli za ofisi, na kwa mawakili wote na watu wengine walioidhinishwa na sheria kuhudhuria au kutekeleza mbele ya Mahakama;

(j) hali ya kawaida ya kimaumbile;

(k) maana ya maneno;

(l) mambo yote ya jumla au yenye sifa mbaya;

(m) mambo yote ambayo yameelekezwa na sheria kupata utambuzi wa kimahakama.

(2) Katika kesi zote hizi zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na pia masuala ya historia ya umma, fasihi, sayansi au sanaa, Mahakama inaweza kutumia kwa msaada katika vitabu muwafaka au nyaraka za kumbukumbu.

(3) Iwapo Mahakama imeombwa na mtu yeyote kuchukua utambuzi wa kimahakama juu ya tukio lolote na inaweza kukataa kufanya hivyo isipokuwa au mpaka mtu huyo atoe kitabu chochote hicho au waraka kama itakavyokuwa muhimu kumuwezesha kufanya hivyo.

Matukio yaliyokubaliwa hayahitaji kuthibitishwa.

63.-(1) Hakuna tukio linalohitaji kuthibitishwa katika mwenendo wowote wa kesi ambapo wadaawa hao au mawakala wao wameyakubali wakati wa kuskilizwa, au ambalo, kabla ya kuskilizwa , walikubaliana kukukubali kwa maandishi yoyote yaliyosainiwa nao au ambayo kwa kanuni yoyote au mashtaka yaliyopo wakati ambapo yanachukuliwa kuwa yamekubaliwa katika madai yao.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mahakama inaweza, kwa uwezo wake, kuhitaji matukio yaliyokubaliwa kuthibitishwa vyenginevyo kuliko kwa kukiri huko.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
USHAHIDI WA MDOMO

Uthibitisho wa matukio kwa ushahidi wa mdomo.

64. Matukio yote, isipokuwa yaliyomo kwenye nyaraka au kumbukumbu za kielektroniki, yanaweza kuthibitishwa kwa ushahidi wa mdomo.

Ushahidi wa mdomo lazima uwe wa moja kwa moja.

65.-(1) Ushahidi wa mdomo lazima, katika hali yoyote itakavyokuwa, uwe wa moja kwa moja, kwamba:

(a) ikiwa unahusisha tukio ambalo lingeweza kuonekana, ni lazima uwe ushahidi wa shahidi anaesema kuwa aliliona;

(b) ikiwa unahusisha tukio ambalo lingeweza kusikika, ni lazima uwe ushahidi wa shahidi anayesema kuwa alilisikia;

(c) ikiwa unahusisha tukio ambalo lingeweza kuhisiwa kwa kiungo chochote cha hisia au kwa njia nyengineyo yoyote, ni lazima uwe ushahidi wa shahidi anayesema amehisi kwa hisia hiyo au kwa namna hiyo; au

(d) ikiwa unahusisha maoni au sababu ambazo maoni hayo yangeweza kutolewa, ni lazima uwe ushahidi wa mtu ambae ana maoni hayo kwa misingi hiyo.

(2) Maoni ya wataalamu yaliyoelezwa katika mkataba wowote wa kimataifa uliotolewa kwa ajili ya kuuzwa, na sababu ambazo maoni hayo yameweza kufikiwa, yanaweza kufikiwa kama mfanyaji wa mkataba huo amefariki au hawezi kupatikana, au hawezi kuitwa kama shahidi bila kupelekea kuchelewa au gharama ambayo Mahakama itaona hayana msingi.

(3) Ikiwa ushahidi wa mdomo unahusiana na kuwepo au sharti la jambo lolote la msingi lisilokuwa hati, Mahakama inaweza, ikiona inafaa kuhitaji kutolewa kitu hicho cha msingi kwa ajili ya ukaguzi wake.

Ushahidi wa mikutano ya video au njia nyenginezo.

66. Mahakama inaweza kuruhusu kutolewa ushahidi, ikiwa ndani au nje ya Zanzibar kwa njia ya video ya moja kwa moja au kwa njia nyenginezo.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
USHAHIDI WA WARAKA

Uthibitisho wa maudhui ya nyaraka.

67. Maudhui ya nyaraka yanaweza kuthibitishwa aidha kwa ushahidi halisi au kwa ushahidi unaotolewa kwa kukosekana ushahidi halisi.

Ushahidi halisi.

68.-(1) Ushahidi halisi maana yake ni waraka halisi ambao umetolewa kwa ukaguzi wa Mahakama.

(2) Wakati waraka umesainiwa katika sehemu kadhaa kila sehemu ni ushahidi halisi wa waraka.

(3) Pale ambapo waraka umesainiwa katika nakala zaidi ya moja kila nakala iliyosainiwa na mmoja au baadhi ya wadaawa, kila nakala ni ushahidi halisi dhidi ya upande uliousaini.

(4) Pale ambapo nyaraka zimefanywa kwa njia iliyo sawa kama vile kunakili au kutoa ronyo au picha, kila moja ni ushahidi halisi wa maudhui yaliyobakia; lakini iwapo kuna nakala zote za nakala halisi, zote hazitokuwa ushahidi halisi wa maudhui ya asili.

Ushahidi usiokuwa halisi.

69. Ushahidi usiokuwa halisi maana yake ni:

(a) nakala zilizothibitishwa zilizotolewa chini ya masharti yaliyoelezwa humu;

(b) nakala zilizofanywa kutoka hati ya asili kwa njia ya mitambo ambayo yenyewe inahakikisha usahihi wa nakala, na nakala zilizoliganishwa na nakala hizo;

(c) nakala zilizofanywa kutokana au kwa kulinganishwa na za asili;

(d) nakala zaidi ya moja za nyaraka dhidi ya pande ambazo hazikutia saini;

(e) hesabu ya mdomo ya maudhui ya waraka uliotolewa na mtu ambae yeye mwenyewe ameiona.

Uthibitisho wa nyaraka kwa ushahidi halisi.

70. Nyaraka lazima zithibitishwe kwa ushahidi halisi isipokuwa katika hali ambazo zimetajwa humu.

Kesi ambazo ushahidi usio halisi unaohusiana na nyaraka unaweza kutolewa.

71.-(1) Ushahidi usio halisi unaweza kutolewa kwa kuwepo, masharti au maudhui ya waraka katika mambo yafuatayo:

(a) ikiwa waraka halisi umeonyeshwa au imetokezea umo katika miliki au uwezo wa:

(i) mtu ambae waraka huo unaombwa kuthibitishwa dhidi yake;

(ii) mtu ambae hawezi kupatikana, au hawezi kuitwa kwa hatua za Mahakama; au

(iii) mtu anaelazimika kisheria kuitoa, na iwapo, baada ya notisi zilizotajwa ndani ya kifungu cha 74 cha Sheria hii, mtu huyo hatoitoa.

(b) iwapo kuwepo, masharti au maudhui ya waraka halisi yamethibitishwa ikikubaliwa kwa maandishi na mtu ambae inathibitishwa dhidi yake au kwa muwakilishi wake ki maslahi;

(c) ikiwa hati halisi imeharibiwa au imepotea, au upande unaotoa ushahidi wa maudhui yake hauwezi, kwa sababu nyengine yoyote isiyotokana na kosa au uzembe wake, kuutoa katika muda muafaka;

(d) ikiwa hati halisi kwa uasili wake haiwezi kuhamishika kirahisi;

(e) ikiwa hati halisi ni waraka wa umma kwa maana ya kifungu cha 84 cha Sheria hii;

(f) ikiwa hati halisi ni nakala ya waraka ulioyothibitishwa umeruhusiwa na Sheria hii, au kwa sheria nyengine yoyote inayotumika ndani ya Zanzibar kwa kutolewa katika ushahidi;

(g) ikiwa hati halisi imejumuisha hesabu kadhaa au nyaraka nyenginezo ambazo haziwezi kuchunguzwa kwa urahisi ndani ya Mahakama, na matukio ya kuthibitishwa ni matokeo ya jumla ya mkusanyiko wote.

(2) Katika aya ya (a), (c) na (d) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ushahidi wowote usio kuwa halisi wa maudhui ya waraka unakubalika.

(3) Katika aya ya (b) ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, kukiri kwa maandishi kunakubalika.

(4) Katika aya ya (e) au (f) vya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, nakala ya waraka iliyothibitishwa, lakini hakuna aina nyengine ya ushahidi inayokubalika.

(5) Katika aya ya (g) ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, ushahidi unaweza kutolewa kwa matokeo ya jumla ya nyaraka na mtu yeyote aliyezichunguza, na mwenye ujuzi katika kuchunguza nyaraka hizo.

Masharti maalum yanayohusiana na kumbukumbu za kielektroniki.

72. Maudhui ya kumbukumbu za kielektroniki yanaweza kuthibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 73 cha Sheria hii.

Kukubalika kwa kumbukumbu za kielektroniki.

73.-(1) Bila ya kujali jambo lolote katika Sheria hii, taarifa yoyote iliyomo katika kumbukumbu za kielektroniki ambayo imenakiliwa katika karatasi, kuhifadhiwa, kurikodiwa au kunakiliwa katika kioo au chombo cha kunasa habari kilichotolewa kwa kompyuta ambayo inajulikana kama vifaa vya kompyuta itachukuliwa kuwa pia ni waraka, iwapo masharti yaliyotajwa katika kifungu hiki yamethibitishwa kuhusiana na taarifa na kompyuta husika na itakubalika katika mienendo yoyote ya kesi bila uthibitisho wa ziada au kutolewa kwa hati halisi, kama ushahidi wa maudhui wa hati halisi au wa tukio lolote lililotajwa ndani yake ambalo ushahidi wa moja kwa moja ungekubalika.

(2) Masharti yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kuhusiana na na vifaa vya kompyuta yatakuwa;

(a) vifaa vya kompyuta vyenye taarifa zilizotolewa na kompyuta kipindi ambacho kompyuta ilikuwa inatumika mara kwa mara kuhifadhi na kushughulikia taarifa kwa madhumuni ya shughuli zozote ambazo kikawaida hufanywa mara kwa mara katika kipindi hicho na mtu ambae anaudhibiti wa kisheria juu ya matumizi ya kompyuta hio;

(b) katika kipindi hicho, taarifa za aina zilizomo katika kumbukumbu za kielektroniki au za aina ambazo taarifa hizo zilizomo zimekuwa zikiingizwa katika kompyuta katika shughuli hizo za kawaida;

(c) katika kipindi chote husika cha muda huo, kompyuta ilikua inafanya kazi ipasavyo au, ikiwa haifanyi kazi ipasavyo, ikiwa haifanyi kazi ipasavyo kwa mda wowote au ilikua haifanyi kazi katika sehemu ya muda huo, haingeweza kuathiri kumbukumbu za kielektroniki au usahihi wa maudhui yake; na

(d) taarifa zilizomo katika kumbukumbu za kielektroniki zimetoka au zimetolewa kutokana na taarifa hizo zilizoingizwa katika kompyuta katika utekelezaji wa kawaida wa shughuli husika.

(3) Iwapo katika kipindi chochote, kazi ya kuhifadhi au kuzishughulikia taarifa kwa madhumuni ya shughuli zozote zinazotekelezwa kikawaida kwa kipindi chote kama kilivyotajwa katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki imefanyiwa kazi kikawaida na kompyuta, ikiwa:

(a) kwa mchanganyiko wa kompyuta zinazofanya kazi muda wote wa kipindi hicho;

(b) kwa kompyuta tofauti zinazofanya kazi kwa kubadilishana kwa kipindi hicho;

(c) kwa mchanganyiko wa kompyuta tofauti ambazo zinafanya kazi kwa kubadilishana kwa muda wa kipindi hicho;

(d) katika hali nyengine yoyote inayohusisha kubadilishana ufanyaji wa kazi wa kompyuta hizo kwa kipindi hicho, katika utaratibu wowote, wa kompyuta moja au zaidi na mchanganyiko wa kompyuta moja au zaidi,

Kompyuta zote zilizotumika kwa dhumuni hilo katika kipindi hicho itachukuliwa kwa madhumuni ya kifungu hiki kama ni kompyuta moja, na rejea katika kifungu hiki kuhusu kompyuta itatumika ipasavyo.

(4) Katika mienendo yoyote ya kesi itakapotakiwa kutolewa maelezo katika ushahidi kwa mujibu wa kifungu hiki, ruhusa inayomruhusu kufanya jambo lolote kati ya yafuatayo:

(a) kutambua kumbukumbu za kieletroniki zinazojumuisha maelezo na zinazoelezea namna ambavyo imetolewa;

(b) inatoa maelezo ya kifaa chochote kilichotumika katika utoaji wa kumbukumbu hizo za kielektroniki kama itakavyoonekana inafaa kwa lengo la kuonesha kwamba kumbukumbu hizo za kieletroniki zimetolewa na kompyuta; au

(c) inayohusiana na mambo yoyote ambayo masharti yake yametajwa na kuhusishwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki,

na kuchukuliwa kuwa imesainiwa na mtu mwenye dhamana ya nafasi inayohusiana na utendaji wa kifaa husika au usimamizi wa shughuli zinazohusika, ambayo yoyote inayofaa, itakuwa ni ushahidi wa jambo lolote lililotajwa katika ruhusa hiyo; na kwa madhumuni ya kifungu kidogo hiki itatosheleza kwa jambo linalotakiwa kutajwa kwa kadri anavyojua na kuamini mtu aliyeeleza jambo hilo.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki;

(a) taarifa zitachukuliwa kuwekwa katika kompyuta kama imesambazwa katika kompyuta hiyo katika mfumo unaokubalika na kama imesambazwa moja kwa moja au, pamoja au bila kuingiliwa kwa binaadamu, kwa kutumia kifaa chochote muafaka;

(b) iwapo katika utendaji wa shughuli taarifa yoyote ya kiofisi imesambazwa ili ihifadhiwe au kufanyiwa kazi kwa ajili ya shughuli hizo inayofanya kazi vyenginevyo isiokuwa ndani ya shughuli hizo, taarifa hiyo, iwapo imesambazwa ipasavyo kwa kompyuta hiyo, itachukuliwa kuwa imesambazwa ndani ya kompyuta hiyo katika utekelezaji wa shughuli hizo;

(c) kinachotokana na kompyuta kitachukuliwa kuwa kimezalishwa na kompyuta kama imetolewa na komyputa hiyo moja kwa moja au, kwa au bila ya kuingiliwa na binaadamu, kwa njia yoyote kifaa muafaka.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, rejea yoyote ya taarifa iliyotolewa kutoka katika taarifa nyengine, itakuwa ni rejea yake iliyotokana nayo kimahesabu, kiulinganisho au njia nyengine yoyote.

Taratibu za notisi ya kutoa hati.

74.-(1) Ushahidi usiokuwa halisi wa maudhui ya nyaraka zilizotajwa katika aya ya (a) (1) ya kifungu cha 71 cha Sheria hii, hautotolewa isipokuwa upande unaopendekeza kutoa ushahidi huo usio halisi hapo awali ulitoa notisi ya kutolewa kwake kwa upande wenye kushikilia waraka huo au wakili wake au wakala, kama ilivyoelezwa na sheria na kama hakuna notisi iliyotajwa kisheria, notisi hiyo kama Mahakama itakavyoona inafaa kwa mazingira ya kesi hiyo.

(2) Notisi iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki haitohitajika ili kuufanya ushahidi huo usiohalisi katika hali yoyote kati ya zifuatazo, au katika hali nyengine ambayo Mahakama itaona inafaa kuzitolea maamuzi:

(a) pale ambapo waraka unaotaka kuthibitishwa wenyewe ni notisi;

(b) pale ambapo mazingira halisi ya kesi, upande kinzani lazima ujuwe kwamba utatakiwa kutoa waraka huo;

(c) pale ambapo itatokea au itathibitika kwamba upande kinzani umeshikilia waraka halisi kwa njia ya udanganyifu au nguvu;

(d) pale ambapo upande kinzani au wakala wake ana waraka halisi katika Mahakama;

(e) pale ambapo upande kinzani au wakala wake amekiri kupokea kwa waraka huo;

(f) pale ambapo mtu mwenye kushikilia waraka huo hapatikani au hahusiki, na utaratibu wa Kimahakama.

Kuthibitishwa saini na mwandiko wa mtu anayedaiwa kusaini au kutolewa waraka ulioandikwa.

75. Ikiwa waraka unaodaiwa kusainiwa au kuandikwa wote au sehemu yake na mtu yeyote, sahihi au muandiko katika waraka huo kama inavyodaiwa kuwa ni muandiko wa mtu huyo lazima ithibitishwe kuwa ni muandiko wake.

Uthibitisho wa saini ya kidigitali.

76. Isipokuwa katika kulinda saini ya kidigitali, ikiwa saini ya kidigitali ya muwekaji yeyote inadaiwa kuwekwa katika kumbukumbu za kielektroniki ukweli kwamba sahihi ya kidigitali ni sahihi ya muwekaji lazima ithibitishwe.

Uthibitisho wa kusainiwa waraka unaohitaji kushuhudiwa kisheria.

77-(1) Ikiwa waraka unatakiwa na sheria kushuhudiwa, hautotumika kama ni ushahidi mpaka mmoja wa mashahidi aliyeshuhudia angalau awe ameitwa kwa ajili ya kuthibitisha kutiwa saini kwake, kama kuna shahidi aliyeshuhudia ambae yuko hai na kwa sharti kwamba taratibu za kimahakama na kuweza kwake kutoa ushahidi.

(2) Haitalazimika kumwita shahidi anayeshuhudia uthibitisho wa utiwaji saini wa waraka wowote, usiokuwa wasia, ambao umesajiliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, isipokuwa kutiwa kwake saini na mtu anayedaiwa kuwa amesaini, kwenyewe kunakanushwa.

Uthibitisho pale ambapo shahidi aliyeshuhudia hapatikani.

78. Iwapo hakuna shahidi aliyeshuhudia anayeweza kupatikana au pale ambapo shahidi hahusiki na taratibu za Mahakama au hana uwezo wa kutoa ushahidi, ni lazima ithibitishwe kwamba ushuhuda wa shahidi mmoja aliyeshuhudia angalau mwandiko wake upo na kwamba saini ya mtu aliyesaini waraka huo mna mwandiko wake.

Kukubalika kwa saini ya mtu aliyeshuhudia waraka.

79. Kukubali kwa upande ulioshuhudia waraka juu ya kutiwa kwake saini na yeye mwenyewe ni uthibitisho wa kutosha dhidi yake wa kusainiwa ingawa ni waraka unaotakiwa na sheria kushuhudiwa.

Uthibitisho ambapo shahidi aliyeshuhudia anakanusha kutiwa saini.

80. Ikiwa shahidi aliyeshuhudia anakanusha au hakumbuki kutiwa saini kwa waraka huo, kutiwa saini kwake kunaweza kuthibitishwa kwa ushahidi mwengine.

Uthibitisho wa waraka ambao hautakiwi kisheria kushuhudiwa.

81. Waraka ulioshuhudiwa ambao hautakiwi kushuhudiwa unaweza kuthibitishwa ikiwa kama waraka huo haukushuhudiwa.

Ulinganisho wa saini, muandiko au muhuri na vyengine uliokubalika au kuthibitishwa.

82.(1) Kwa madhumuni ya kuthibitisha ama saini, maandishi au muhuri kuwa ni ya mtu anayedaiwa kuiandika au kufanya, sahihi yoyote, muandiko au muhuri wowote uliokubaliwa au kuthibitishwa na Mahakama kuwa uliandikwa au ulifanywa na mtu huyo unaweza kulinganishwa na ule ambao unataka kuthibitishwa, ingawa saini hiyo, maandishi au muhuri haukutolewa au kuthibitishwa kwa madhumuni yoyote mengine.

(2) Mahakama inaweza kutoa miongozo kwa mtu yeyote aliyekuwepo Mahakamani kuandika maneno yoyote au namba kwa madhumuni ya kuiwezesha Mahakama kulinganisha maneno au namba zilizoandikwa na maneno yoyote au namba zinazodaiwa kuandikwa na mtu huyo.

Kifungu hiki pia kitatumika, kwa marekebisho yoyote yatakayolazimu, kwa muonekano wa kidole au kidole gumba.

Uthibitisho juu ya usahihi wa saini ya Kidigitali.

83.-(1) Ili kuhakikisha saini ya kidigitali ni ya mtu ambaye anapaswa kuiweka, Mahakama inaweza kuelekeza

(a) mtu au mdhibiti au mamlaka ya kuthibitisha kutoa cheti cha saini ya kidigitali;

(b) mtu mwengine yeyote kutumia nambari ya siri ya umma zilizoorodheshwa katika cheti cha saini ya kidigitali na kuhakikisha saini ya kidigitali inayodaiwa kuwekwa na mtu huyo;

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "Mdhibiti" maana yake ni mdhibiti wa mamlaka za kuthibitisha aliyeteuliwa na Waziri anaehusika na masuala ya TEHAMA.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
NYARAKA ZA UMMA

Nyaraka za Umma.

84. Nyaraka zifuatazo ni Nyaraka za Umma:

(a) nyaraka zinazofanya matendo au kumbukumbu za matendo ya:

(i) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) vyombo rasmi na mabaraza ya usuluhishi na;

(iii) watumishi wa umma, mamlaka za kutunga sheria, mahakama na chombo cha utendaji, zikiwa za Zanzibar au sehemu yoyote ya Jamhuri ya muungano ya Tanzania au nchi ya kigeni.

(b) kumbukumbu za umma zilizohifadhiwa Zanzibar ambazo ni nyaraka binafsi.

Nyaraka binafsi.

85. Nyaraka zote ambazo hazikutajwa katika kifungu cha 84 cha Sheria hii, ni nyaraka binafsi.

Nakala za nyaraka za Umma zilizothibitishwa.

86.-(1) Afisa wa umma ambae atakuwa na udhibiti wa nyaraka za umma, ambapo mtu yeyote yule ana haki ya kuichunguza, atampa mtu huyo nakala ya nyaraka hiyo atakapohitaji, baada ya kufanya malipo yanayohitajika, pamoja na cheti kilichoandikwa katika nakala hiyo kuwa ni nakala ya kweli ya nyaraka hiyo au sehemu yake, kama itakavyokuwa, na vyeti hivyo vitakuwa na tarehe na kusainiwa na Afisa huyo kwa jina lake na cheo chake, na kitawekwa muhuri, pale ambapo afisa huyo ameidhinishwa na sheria kutumia muhuri, na nakala hizo zilizothibitishwa zitaitwa nakala zilizothibitishwa.

(2) Afisa ambae, katika utendaji wa kazi yake, ana mamlaka ya kutoa nakala hizo, atakuwa na dhamana ya nyaraka hizo katika maana ya kifungu hiki.

Uthibitisho wa Nyaraka kwa kutoa hati zilizothibitishwa.

87. Nakala zilizothibitishwa zilizotajwa katika kifungu cha 86 cha Sheria hii zinaweza kutolewa katika kuthibitisha maudhui yaliyomo katika Nyaraka za Umma au sehemu ya Nyaraka za Umma ambayo inadaiwa kuwa ni nakala.

Uthibitisho wa Nyaraka nyingine Rasmi.

88. Nyaraka za Umma zifuatazo zinaweza kuthibitishwa kama ifuatavyo:

(a) sheria, amri au taarifa zinazohusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Idara zake zozote:

(i) kwa kumbukumbu za idara, zilizothibitishwa na wakuu wa idara husika; au;

(ii) kwa waraka wowote unaodaiwa kunakiliwa kwa amri ya Serikali

(b) kwa mwenendo wa Mabaraza ya kutunga sheria ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kikanda au Mashirika ya Kimataifa na kwa majarida ya vyombo hivyo husika au sheria zilizochapishwa au muhtasari, au kwa nakala, zinazodaiwa kuchapishwa kwa amri ya Serikali;

(c) matamko, amri au kanuni zilizotolewa na Rais wa Zanzibar au wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Idara yoyote ya Serikali ya Zanzibar au Idara yoyote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nakala au dondoo zilizomo katika Gazeti rasmi au zinazodaiwa kunakiliwa na Mchapishaji wa Serikali;

(d) matendo ya chombo cha utawala au kwa mwenendo wa Bunge la nchi ya kigeni, Kikanda au Mashirika ya Kimataifa, kwa majarida yaliyochapishwa kwa mamlaka yao, au yanayopokelewa kwa kawaida katika nchi hiyo, au kwa nakala iliyothibitishwa kwa mhuri wanchi au dola, au kwa utambuliwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au, za Zanzibar;

(e) mwenendo wa chombo cha Manispaa, ndani ya Zanzibar au ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nakala iliothibitishwa na mtunzaji wa Sheria, au kwa kitabu kinachodaiwa kuchapishwa na mamlaka ya chombo hicho;

(f) nyaraka za umma za tabaka jengine lolote katika nchi ya kigeni, nyaraka halisi, au kwa nakala iliyothibitishwa na mtunzaji wa sheria, kwa hati yenye mhuri wa mkuu wa viapo au wakala wa kidiplomasia, kwamba na nakala hiyo imethibitishwa ipasavyo na Afisa mwenye udhibiti kisheria wa nyaraka halisi na kwa uthibtisho wa sifa ya nyaraka kulingana na sheria za nchi ya kigeni.

SEHEMU YA KUMI NA NNE
DHANA JUU YA NYARAKA

Dhana juu ya uhalali wa nakala zilizothibitishwa.

89.-(1) Mahakama itajaalia kuwa ni halisi kila waraka unaodaiwa kuthibitishwa, nakala iliothibitishwa au waraka mwengine ambao kwa mujibu wa sheria unatajwa kukubalika kama ushahidi wa maelezo yoyote ya tukio na ambao unadaiwa kuthibitishwa ipasavyo na afisa yeyote ndani ya Zanzibar ambae ameidhinishwa kwa ajili hiyo:

Isipokuwa kwamba, waraka huo kimsingi upo katika muundo na unadaiwa kusainiwa kwa namna ilivyoelekezwa na sheria kwa ajili hiyo.

(2) Mahakama pia itachukulia/itajaalia kuwa afisa yeyote ambae atasaini au kuthibitisha nyaraka hiyo, wakati anatia saini nyaraka hiyo ana wadhifa uliotajwa kwenye nyaraka hiyo

Dhana juu ya nyaraka zinazotolewa kama kumbukumbu ya ushahidi.

90.-(1) Nyaraka inapotolewa katika Mahakama yoyote ile ili iwe kama kumbukumbu au mtiririko wa ushahidi, au sehemu yoyote ile ya ushahidi, utakaotolewa na shahidi wakati wa mwenendo wa kesi au mbele ya Afisa yeyote yule mwenye mamlaka kisheria kuchukua ushahidi huo kuwa ni maelezo au ungamo la mshitakiwa, lililochukuliwa kwa mujibu wa sheria, na kudaiwa kusainiwa na Jaji yeyote au Hakimu, au afisa yeyote kama ilivyotajwa Mahakama itajaalia kwamba:

(a) waraka huo ni halisi;

(b) maelezo yoyote katika mazingira ambayo yalichukuliwa, yakidaiwa kufanywa na mtu aliyeyasaini, ni kweli; na

(c) ushahidi huo, maelezo au ungamo lilichukuliwa ipasavyo.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na sheria nyengine yoyote, iwapo katika mwenendo wa kesi za jinai inajumuisha kosa la ugaidi au ugaidi wa kimataifa, swali linaibuka kama jambo lolote au kitu kipo katika hali iliyoelezwa au kudaiwa kuelezwa katika waraka, waraka huo utakubalika katika ushahidi bila ya uthibitisho wa saini au mamlaka ya mtu aliyejitokeza kuisaini na iwapo hakuna ushahidi unaokinzana, utakuwa uthibitisho wa matukio yaliyotajwa ndani yake.

Dhana juu ya Gazeti rasmi la serikali, magazeti, sheria za baraza la kutunga sheria na Nyaraka nyenginezo.

91.-(1) Mahakama itajaalia uhalali wa kila nyaraka unaodaiwa kuwa ni Gazeti Rasmi, au Gazeti Rasmi la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, au kuwa gazeti au jarida, au kuwa nakala ya sheria ya Baraza la Wawakilishi iliyochapishwa na Mpiga Chapa wa Serikali, na wa kila waraka unaodaiwa kuwa ni waraka ulioelekezwa na sheria yoyote kuhifadhiwa na mtu yeyote, iwapo waraka umehifadhiwa kimsingi katika muundo uliotakiwa na sheria na umetolewa kutoka kwa udhibiti muwafaka.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki,waraka unadaiwa kuwa katika udhibiti sahihi iwapo uko katika mahala ambapo, na katika uangalizi wa mtu ambae uangalizi wake kwa kawaida ungepaswa kuwa wa kawaida.

(3) Udhibiti huo hautochukuliwa kutokuwa sahihi ikiwa itathibitika kuwa na uhalali wa asili, au iwapo mazingira ya kesi ni kwamba kufanya uasili huo kukubalika.

Dhana kuhusiana na gazeti rasmi katika mfumo wa kielektroniki.

92. Mahakama itadhania uhalisia wa kila rekodi ya kielektroniki inayodaiwa kuwa ni Gazeti Rasmi au inayodaiwa kuwa ni kumbukumbu ya kielektroniki iliyoelekezwa na sheria yoyote kwa lengo la kuhifadhiwa na mtu yeyote, ikiwa kumbukumbu hiyo ya kielektroniki imehifadhiwa kwa sehemu kubwa katika mfumo unaotakiwa na sheria na inatolewa kutoka kwa udhibiti sahihi.

Dhana kuhusiana na ukusanyaji wa sheria na ripoti za maamuzi.

93. Mahakama itachukulia uhalali wa kila kitabu kinachodaiwa kunakiliwa au kuchapishwa chini ya mamlaka ya Serikali ya nchi yoyote, na kuwa na sheria za nchi hiyo, na ya kila kitabu kinachodaiwa kuwa na ripoti ya maamuzi ya Mahakama ya nchi hiyo.

Dhana kuhusiana na ramani au michoro iliyofanywa na mamlaka ya Serikali.

94. Mahakama italazimika kuchukulia na kuamini kwamba nyaraka inayotarajiwa kufanya kazi nje ya Zanzibar inaweza kufanya kazi na ufanyaji wake kazi utakubaliwa bila ya kutiliwa mashaka ya aina yoyote ikiwa nyaraka hiyo itasainiwa na muhusika na kuwekwa muhuri na Hakimu, Mrajisi wa Mahakama, Jaji, Mkuu wa viapo, Afisa wa mambo ya nje wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania au mwakilishi yeyote wa kibalozi au Katibu yeyote anayeiwakilisha nchi au mtu yeyote katika nchi ya kigeni ambaye ataidhinishwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria za nchi husika kuthibitisha nyaraka hiyo.

Dhana kuhusiana na nyaraka binafsi zilizofanywa nje ya Zanzibar.

95. Mahakama itajaalia kwamba nyaraka binafsi inayodaiwa kufanywa nje ya Zanzibar ilifanywa kwa usahihi na kuthibitishwa ipasavyo iwapo:

(a) kuhusiana na waraka uliofanywa Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Malawi au Zambia, inadaiwa kuthibitishwa na Hakimu, Mrajisi au Jaji ikiwa na muhuri wa Mahakama au Mkuu wa viapo kwa sahihi yake na muhuri wa ofisi.

(b) kuhusiana na waraka uliosainiwa Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Malawi au Zambia ambao unaathiri au unahusu mali isiyozidi kiasi au thamani ya shilingi elfu tano, unadaiwa kuambatanishwa na au kuingizwa katika waraka huo taarifa iliyosainiwa na hakimu au mlinzi wa amani:

(i) kwamba mtu anayesaini waraka huo ni mtu anaemjua;au

(ii) kwamba watu wengine wawili ambao Hakimu au Mlinzi wa Amani anawajuwa na kila mmoja amemthibitishia Hakimu au Mlinzi wa Amani kuwa wanamfahamu mtu aliyefanya waraka huo.

(c) kuhusiana na waraka uliofanywa mahala pengine popote nje ya Zanzibar, iwapo inadaiwa kuthibitishwa kwa saini na muhuri wa:

(i) afisa wa ubalozi wa Jamhuri ya Muungano au mwakilishi wa kidiplomasia wa nchi za Jumuia ya Madola katika sehemu hiyo au;

(ii) Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje au mtu mwengine katika nchi ya kigeni, ambae ataoneshwa kwa uthibitisho wa afisa wa ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au mwakilishi wa kidiplomasia wa nchi za Jumuiya ya Madola katika mahala hapo kuwa ameruhusiwa kwa mujibu wa sheria za sehemu hiyo, kuthibitisha nyaraka.

Dhana kuhusiana na hati ya uwakala.

96. Mahakama itajaalia kwamba kila waraka unaodaiwa kuwa ni hati ya uwakala na uliosaniwa na kuthibitishwa na Mkuu wa viapo au Jaji, Hakimu au Mrajis, afisa wa ubalozi au mwakilishi wa kidiplomasia wa nchi ya Jumuiya ya Madola, umesainiwa na kuthibitishwa hivyo.

Dhana juu ya makubaliano ya kielektroniki.

97. Mahakama itajaalia kwamba kila kumbukumbu ya kielektroniki inayodaiwa kuwa ni makubaliano yenye saini za kidigitali za wadaawa uliingiwa kwa kuweka saini za kidigitali za wadaawa.

Dhana juu ya kumbukumbu za kielektroniki na saini za kidigitali.

98.-(1) Katika mwenendo wa kesi yoyote ile itakayohusisha uwekaji wa kumbukumbu ya kielektroniki, Mahakama itajaalia kwamba isipokuwa ikithibitika vyenginevyo, kwamba kumbukumbu iliyowekwa ya kidigitali haijabadilishwa tokea muda ambao saini hiyo inahusika.

(2) Katika mwenendo wowote unaohusisha uwekaji saini ya kidigitali, isipokuwa ikithibitika vyenginevyo, Mahakama itajaalia kwamba:

(a) saini iliyowekwa ya kidigitali imewekwa na muwekaji kwa nia ya kusaini au kuthibitisha kumbukumbu za kielektroniki;

(b) isipokuwa katika uwekaji wa kumbukumbu ya kielektroniki au saini ya kidigitali, hakuna chochote katika kifungu hiki kitakacholeta dhana kuhusiana na usahihi na hadhi ya kumbukumbu za kielektroniki au saini yoyote ya kidigitali.

Dhana kuhusiana na Vyeti vya saini ya kidigitali.

99. Mahakama itajaalia kuwa, isipokuwa kama itathibitishwa vyenginevyo, taarifa iliyoorodheshwa katika cheti cha saini ya kidigitali ni sahihi, isipokuwa kwa taarifa zilizorejeshwa kama taarifa za mtiaji saini ambazo hazikuthibitishwa, iwapo cheti hicho kilipokelewa na mtiaji saini.

Dhana kuhusiana na nakala zilizothibitishwa za kumbukumbu za mahakama ya kigeni.

100. Mahakama itajaalia kwamba waraka wowote unaodaiwa kuwa nakala iliyothibitishwa ya kumbukumbu yoyote ya mahakama ya nchi ya kigeni ni halali na sahihi, iwapo waraka unaodaiwa kuthibitishwa kwa hali yoyote ambayo imethibitishwa na afisa wa ubalozi wa kigeni au mwakilishi wa kidiplomasia wa nchi ya Jumuiya ya Madola kuwa njia ambayo kwa kawaida itatumika katika nchi kwa kuthibitisha nakala za kumbukumbu za Mahakama.

Dhana kuhusiana na vitabu, ramani na michoro.

101. Mahakama itajaalia kwamba kitabu chochote ambacho kinaweza kufanya rejea kwa taarifa kuhusiana na mambo ya umma au maslahi ya jumla, na kwamba ramani au mchoro wowote uliochapishwa ambayo maelezo yake ni matukio yanayohusiana na ambayo yametolewa kwa ukaguzi ziliandikwa na kuchapishwa na mtu huyo na kwa wakati na pahala, ambao unadaiwa kuchapishwa au kuandikwa.

Dhana kuhusiana na ujumbe wa mawasiliano ya simu.

102. Mahakama itajaalia kwamba ujumbe, uliotumwa kutoka afisi ya mawasiliano ya simu kwa mtu ambae ujumbe huo unadaiwa kutumwa, unawiyana na ujumbe uliotumwa kwa kusambazwa katika ofisi ambayo ujumbe huo unadaiwa kutumwa; lakini Mahakama haitoweka dhana yoyote kwa mtu ambae ujumbe huo ulitumwa kwa kusambazwa.

Dhana kuhusiana na ujumbe wa kielektroniki.

103.-(1) Mahakama inaweza kujaalia kwamba ujumbe wa kielektroniki uliotumwa na mtumaji kwa huduma ya barua pepe kwa anayetumiwa ambaye ujumbe unadaiwa kutumwa kuelekezwa kwake unawiyana na ujumbe kama ulivyowekwa katika kompyuta yake kwa ajili ya usambazaji; lakini Mahakama haitoweka dhana yoyote kuhusiana na mtu ambae ametumiwa ujumbe huo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki;

"mpelekewa" inamaanisha kuwa ni mtu ambae amekusudiwa na mtumaji kupokea kumbukumbu za kielektroniki lakini haijumuishi mtu yeyote wa kati;

"mtumaji" inamaanisha kuwa mtu ambae ametuma, amezalisha, amehifadhi au amesambaza ujumbe wowote wa kielektroniki au anaesababisha ujumbe wowote wa kielektronki kutumwa, kuzalishwa, kuhifadhiwa au kusambazwa kwa mtu mwengine yeyote lakini haitojumuisha mtu wakati.

Dhana kuhusiana na utiaji saini wa nyaraka zisizotolewa.

104. Mahakama itajaalia kwamba kila waraka, uliotakiwa kutolewa na haukutolewa baada ya notisi ya kutolewa, umethibitishwa, umepigwa muhuri na kusainiwa kwa namna inavyotakiwa.

Dhana kuhusiana na nyaraka za miaka thelathini.

105.-(1) Pale ambapo waraka wowote unaodaiwa au kuthibitishwa kuwa ni wa miaka thelathini unatolewa kutoka katika udhibiti wowote ambao Mahakama inaona ni sahihi, Mahakama inaweza kujaalia kwamba saini na kila sehemu nyengine ya waraka huo, ambao unadaiwa ni mwandiko wa mtu yeyote maalum, uko katika mwandiko wa mtu huyo, na iwapo waraka umesainiwa au kushuhudiwa, kwamba ulisainiwa ipasavyo na kushuhudiwa na watu ambao wanadaiwa kusaini na kushuhudiwa.

(2) Nyaraka zinadaiwa kuwa katika udhibiti sahihi ikiwa zipo katika mahala ambapo, na katika uangalizi wa mtu ambae, angepaswa kuwa nazo, lakini hakuna udhibiti utakaokuwa si sahihi ikiwa itathibitika kuwa uasili halali, au iwapo mazingira ya kesi maalumu ni kwamba inapelekea kuwa wa asili.

Dhana kuhusiana na kumbukumbu za kielektroniki za miaka mitano.

106.-(1) Pale ambapo kumbukumbu yoyote ya kielektroniki, inayodaiwa au kuthibitika kuwa na miaka mitano, inatolewa katika himaya yoyote ambayo Mahakama katika mazingira maalumu inaona inafaa, Mahakama inaweza kujaalia kwamba saini ya kidigitali ambayo inadaiwa kuwa ni saini ya kidigitali ya mtu maalum ambae iliwekwa na yeye au mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa kwa ajili hiyo.

(2) Kumbukumbu za kielektroniki zinazodaiwa kuwa katika udhibiti sahihi iwapo zipo katika mahala ambapo na katika uwangalizi wa mtu ambae, angepaswa kuwa nazo lakini hakuna udhibiti usiokuwa sahihi ikiwa utathibitika kuwa kuna uasili halali, au mazingira ya hali maalum ni kwamba inapelekwa kuwa wa asili.

(3) Kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kitatumika kwa kifungu cha 92 cha Sheria hii.

SEHEMU YAKUMI NA TANO
UONDOAJI WA USHAHIDI WA MDOMO
KWA USHAHIDI WA HATI

Ushahidi wa masharti wa mikataba, utoaji na uhaulishaji mwengine wa mali kwa njia ya waraka.

107.-(1) Wakati masharti ya mkataba au utoaji, au uhaulishaji mwingine wa mali, umewekwa katika muundo wa waraka na katika hali zote ambazo jambo lolote linalotakiwa kisheria kuweko kwa mfumo wa hati, hakuna ushahidi utakao tolewa katika uthibitisho wa masharti ya mkataba huo, utoaji au uhaulishaji mwingine wa mali au wa jambo hilo isipokuwa kwa waraka wenyewe au ushahidi usiokuwa halisi wa maudhui yake katika hali ambayo ushahidi usiokuwa halisi unakubalika chini ya msharti yaliyotanguliwa kutajwa, isipokuwa kwamba;

(a) iwapo afisa wa umma anahitajika na sheria kuteuliwa kwa maandishi, na wakati inaonyeshwa kwamba mtu yeyote maalum ametekeleza akiwa afisa huyo, maandishi ambayo ameteuliwa kwayo hayahitaji kuthibitishwa; na

(b) wasia zilizopokelewa kwa chombo kinachohusiana na usimamizi mirathi katika Zanzibar zinaweza kuthibitishwa na chombo kinachohusiana na usimamizi wa mirathi.

(2) Kifungu hiki kitatumika sawa na mazingira ambayo mikataba, ruzuku au uhaulishaji mali iliyotajwa inaorodheshwa katika waraka mmoja na kwa mazingira ambayo imo katika zaidi ya waraka mmoja.

(3) Pale ambapo kuna nyaraka halisi zaidi ya moja, mmoja tu unahitaji kuthibitishwa.

(4) Maelezo, katika nyaraka zozote ziwazo, za tukio lisilokuwa matukio yaliotajwa katika kifungu hiki, hayatozuia kukubalika kwa ushahidi wa mdomo wa tukio hilo hilo.

Kuondolewa kwa ushahidi wa makubaliano ya mdomo.

108. Iwapo masharti ya mkataba wa aina yoyote, utoaji au uhaulishaji mwingine wa mali, au jambo lolote linalohitajika kisheria kuwekwa katika mfumo wa waraka, umethibitishwa kwa mujibu wa kifungu cha 107 cha Sheria hii, hakuna ushahidi wa makubaliano yoyote ya mdomo au maelezo yatakayokubalika, baina ya wadaawa kwa hati yoyote hiyo au wawakilishi wa kimaslahi, kwa madhumuni ya kupinga, kubadilisha, kuongeza, au kupunguza kutoka kwa masharti yake isipokuwa kwamba:

(a) tukio lolote linaweza kuthibitishwa ambalo lingebatilisha hati yoyote au ambalo lingempasa mtu yeyote kwa amri yoyote inayohusiana nayo; kama vile udanganyifu, kupoteza nguvu, kusikokuwa halali, kuhitajika kusainiwa ipasavyo, kuhitajika kuwa na uwezo kwa upande wowote wa mkataba, haja ya kuwepo au kukosekana kwa maslahi, au kukosea hakika au sheria;

(b) kuwepo kwa makubaliano yoyote tofauti ya mdomo kwa jambo lolote ambalo hati iko kimya na ambalo halipingani na msharti yake kunaweza kuthibitishwa; katika kuzingatia kama angalizo hili linatumika au la, Mahakama itazingatia kiwango cha uandaaji wa hati;

(c) kuwepo kwa makubaliano yoyote tofauti,yenye sharti linalotegemea kutokea kwa hali fulani sharti linalotegemea kuhusiana na jukumu lolote chini ya mkataba wowote huo, utoaji, au uhaulishaji mali, kunaweza kuthibitishwa;

(d) kuwepo kwa makubaliano yoyote tofauti ya baadae ya mdomo ya kusitisha au kurekebisha mkataba wowote huo, utoaji au uhaulishaji mali, kunaweza kuthibitishwa isipokuwa katika mazingira ambayo mkataba huo, utoaji au uhaulishaji mali unatakiwa na sheria kuwa kwa njia ya maandishi, au umesajiliwa kwa mujibu wa sheria inayotumika kwa muda uliopo kuhusiana na usajili wa nyaraka;

(e) matumizi yoyote au desturi ambayo matukio yasiyotajwa kwa uwazi katika mkataba wowote kwa kawaida yanaambatanishwa na mikataba ya aina hiyo, inaweza kuthibitishwa, ikiwa kuambatanishwa kwa matukio hayo haitakuwa kinyume na, au kupingana na, masharti bayana ya mkataba;

(f) tukio lolote linaweza kuthibitishwa ambalo linaonyesha kwa namna gani lugha ya waraka inahusiana na matukio yaliyopo.

Kuondoa ushahidi wa kuelezea au kurekebisha hati yenye utata.

109. Endapo lugha iliyotumika katika waraka, yenyewe, ni tata au mapungufu, ushahidi hauwezi kutolewa kwa matukio ambayo yataonyesha maana yake au kusambaza mapungufu yake.

Kuondoa ushahidi dhidi ya matumizi ya waraka kwa matukio yaliyopo.

110. Wakati lugha iliyotumika katika waraka yenyewe ni yenye kueleweka kwa uwazi, na inapotumika kwa usahihi kwa matukio yaliyopo, ushahidi unaweza usitolewe kuonyesha kwamba haukumaanishwa kutumika kwa matukio hayo.

Ushahidi kuhusiana na waraka usio na maaana kuhusiana na matukio yaliopo.

111. Wakati lugha iliyotumika katika waraka yenyewe ni yenye kueleweka kwa uwazi, lakini haina maana kuhusiana na matukio yaliopo, ushahidi unaweza kutolewa kuonyesha kwamba ulitumika kwa maana ya kipekee.

Ushahidi kuhusiana na matumizi ya lugha kwa kundi moja kati ya makundi mawili ya matukio, yasiyotumika kwa usahihi wa yeyote.

112. Endapo matukio ni kwamba lugha iliyotumika ilimaanisha kutumika kwa mtu mmoja yeyote, na isingeweza kumaanisha kutumika kwa zaidi ya mtu mmoja, kati ya watu au vitu kadhaa, ushahidi unaweza kutolewa kwa matukio ambayo yanaonyesha wapi kati ya watu au vitu hivyo ilikusudiwa kutumika kwayo.

Ushahidi kuhusiana na matumizi ya lugha ambayo ingeweza kutumika kwa mmoja tu kati ya watu kadhaa.

113. Endapo lugha iliotumika, inatumiwa sehemu ya matukio ya aina moja yaliyopo na sehemu nyingine ya matukio ya aina nyengine yaliyopo, lakini kwa ujumla hayatumiki kiusahihi kwa yoyote, ushahidi unaweza kutolewa kuoyesha ipi kati ya sehemu mbili ilimaanishwa kutumika.

Ushahidi kuhusiana na maana ya tabia zisizoeleweka.

114. Ushahidi unaweza kutolewa kuonyesha maana isiyoeleweka au isiyo katika uzoefu wa kawaida, ya kigeni, isiotumika, ya kiufundi, ya kiutamaduni, na maelezo ya kijimbo au ufupisho, na maneno yaliyotumika katika maana ya kipekee.

Nani anaeweza kutoa ushahidi wa makubaliano yanayopingana na masharti ya nyaraka.

115. Watu ambao si wadaawa katika waraka, au wawakilishi wao kimaslahi, wanaweza kutoa ushahidi wa matukio yoyote kwa nia ya kuonyesha makubaliano yaliyopo yanapingana na masharti ya waraka.

Kubakishwa kwa masharti ya sheria ya mirathi kuhusiana na wasia.

116. Hakuna jambo lolote katika sehemu hii litakalochukuliwa kuathiri vifungu vyovyote vya sheria ya mirathi vinavyohusiana na uandaaji wa wasia.

SEHEMU YA KUMI NA SITA
JUKUMU LA KUTHIBITISHA

Jukumu la kuthibitisha.

117.-(1) Yeyote anaetaka Mahakama yoyote kutoa hukumu kuhusiana na haki yoyote ya kisheria au dhima kutegemeana na kuwepo kwa matukio aliyoyataja lazima athibitishe kuwepo kwa matukio hayo.

(2) Wakati mtu anapaswa kuthibitishwa kuwepo kwa tukio lolote, inadaiwa kwamba dhima ya kuthibitisha ipo kwa mtu huyo.

Kwa nani dhima ya kuthibitisha inaangukia.

118. Dhima ya kuthibitisha katika shauri au mwenendo wa kesi, linaangukia kwa mtu ambaye angeshindwa kama hakuna ushahidi ambao ungetolewa na upande wowote.

Dhima ya kuthibitisha tukio maalumu.

119. Dhima ya kuthibitisha kuhusiana na tukio lolote maalum inaangukia kwa mtu ambae anaitaka Mahakama kuamini uwepo wa tukio hilo, isipokuwa kama imeelezwa na sheria yoyote kwamba uthibitisho wa tukio hilo unaangukia kwa mtu yeyote maalum.

Dhima ya kuthibitisha tukio kuthibitishwa kufanya ushahidi ukubalike.

120. Dhima ya kuthibitisha tukio lolote muhimu la kuthibitishwa ili kumuwezesha mtu yeyote kutoa ushahidi wa tukio jengine lolote iko kwa mtu ambae anataka kutoa ushahidi huo.

Kiwango cha dhima ya kuthibitisha kuwa kwa mshitakiwa katika kesi fulani.

121.-(1) Wakati mtu anashtakiwa kwa kosa lolote, dhima ya kuthibitisha kuwepo kwa mazingira yanayopelekea kesi hiyo kuepushwa au msamaha kutoka, au sifa kwa matumizi ya sheria inayofanya kosa aliloshtakiwa nalo, na dhima ya kuthibitisha tukio lolote maalum katika uelewa wa mtu huyo iko juu yake.

(2) Dhima hiyo itachukuliwa kuondoka iwapo Mahakama itaridhika ushahidi uliotolewa na mwendesha mashtaka, ikiwa wakati wa kuhojiwa na upande kinzani au vyenginevyo, kwamba mazingira au matukio hayo yapo.

(3) Mtu aliyeshitakiwa atapaswa kuachiwa kwa kosa aliloshtakiwa nalo ikiwa Mahakama itaridhika kwamba ushahidi uliotolewa ama na upande wa mashtaka au wa utetezi unafanya shaka ya msingi kuhusiana na hatia ya mshtakiwa kwa kosa hilo.

(4) Hakuna jambo lolote katika kifungu hiki ambalo:

(a) linaathiri au kupunguza chochote kuhusiana na jukumu la kuanzisha ushahidi kwa mujibu wa sheria , tendo lolote kuacha kufanya tendo au kwa nia ambayo kisheria ni muhimu kuwezesha kuwepo kosa ambalo mtu ameshtakiwa nalo;

(b) litaweka kwa upande wa mashitaka, dhima ya kuthibitisha kwamba mazingira ambayo au matukio yalioelezewa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayapo; au

(c) litaathiri dhima iliyowekwa kwa mshtakiwa kuthibitisha utetezi wa kulewa au ugonjwa wa akili.

Dhima ya kuthibitisha tukio hasa kwenye uelewa wa kesi za madai.

122. Katika mwenendo wa madai, wakati tukio lolote liko hasa ndani ya uelewa wa mtu yeyote, dhima ya kuthibitisha tukio hilo lipo juu yake.

Dhima ya kuthibitisha kifo cha mtu anaejulikana kuwa alikuwa hai ndani ya miaka thelathini.

123. Wakati suala ni ama mtu yuko hai au amekufa, na inaonyeshwa kwamba alikuwa hai ndani ya miaka thelathini, dhima ya kuthibitisha kwamba amekufa iko kwa mtu anaethibitisha hilo.

Dhima ya kuthibitisha kwamba mtu yuko hai ambae hajasikika kwa miaka saba.

124. Wakati suala ni ama mtu yupo hai au amekufa, na ikathibitishwa kwamba hajasikika kwa muda wa miaka saba kwa watu ambao kwa kawaida wangesikia juu yake kama alikuwa hai, dhima ya kuthibitisha kwamba yuko hai inahamia kwa mtu ambae anathibitisha hilo.

Dhima ya kuthibitisha uhusiano katika kesi ya wabia,mwenye ardhi au mpangaji, mtoa uwakala na wakala.

125. Wakati suala ni ama watu ni wabia, mwenye ardhi na mpangaji, au mtoa uwakala na wakala, na imeonyeshwa kwamba wamekuwa katika mahusiano hayo dhima ya kuthibitisha kwamba hawapo tena katika mahusiano hayo au wamesita, katika mahusiano hayo, ipo kwa mtu ambae anathibitisha hayo.

Dhima ya kuthibitisha umiliki.

126. Wakati suala ni ama mtu yeyote ni mmiliki wa kitu chochote ambacho inaonyesha ni mwenye kukishikilia, dhima ya kuthibitisha kwamba sio mmiliki iko kwa mtu ambae anathibitisha kwamba sio mmiliki.

Uthibitisho wa nia njema katika matendo pale ambapo upande mmoja katika mahusiano ya kujiamini.

127. Pale ambapo suala ni nia njema ya tendo baina ya wadaawa, mmoja kati yao akawa ni mwenye kujiamini, dhima ya kuthibitisha nia njema ya tendo iko kwa upande wa anaejiamini.

Kizazi wakati wa ndoa ni uthibitisho tosha wa uhalali.

128. Tukio kwamba mtu yeyote alizaliwa wakati wa muendelezo wa ndoa halali baina ya mama yake na mwanaume yeyote, au ndani ya siku mia mbili themanini baada ya kuvunjika ndoa, mama akabakia bila ya kuolewa, itakuwa ni uthibitisho tosha kwamba ni mtoto halali wa mwanaume yule isipokuwa kwamba inaweza kuonyeshwa kwamba wana ndoa hawakupata fursa ya kukutana kimwili kati yao kwa mda wote ule wakati alipozaliwa.

Mahakama inaweza kuchukulia uwepo wa matukio fulani.

129. Mahakama inaweza kuchukulia uwepo wa tukio lolote ambalo inadhani huenda lilitokea, zingatio likiwa kwa sababu za kawaida za matukio ya kimaumbile, tabia za kibinaadamu na shughuli za kibiashara za umma na binafsi katika mahusiano yao kwa matukio ya kesi husika.

SEHEMU YA KUMI NA SABA
ZUIO

Zuio.

130. Wakati mtu, kwa tamko lake, tendo au kuacha kutenda, kwa makusudi akasababisha au akaruhusu mtu mwengine kuamini kitu kuwa ni cha kweli na kwa imani hiyo akatenda jambo, si yeye wala mwakilishi wake ataruhusiwa, katika kesi au mwenendo wa kesi yoyote baina yake na mtu huyo mwingine au wakala wake kukanusha ukweli wa jambo hilo.

Mazuio kwa mpangaji, mtu aliye ruhusiwa au mtu aliekalia.

131.-(1) Mpangaji wa mali isiohamishika au mtu anaelalamika kupitia kwa mpangaji huyo hatoruhusiwa wakati anaendelea na upangaji huo, kukanusha kwamba mkodishaji wa ardhi hiyo kwa mpangaji, mwanzoni mwa upangishaji huo, alikuwa na umiliki wa mali hiyo isiyohamishika.

(2) Mtu aliyekuja kwenye mali yoyote isiyohamishika kwa ruhusa ya mtu ambae ni mwenye kuishikilia hataruhusiwa kukanusha kwamba mtu huyo alikua na umiliki wa kushikilia huko wakati ruhusa hiyo ilipotolewa.

Mazuio ya mpokea stakabadhi ya malipo, mdhaminiwa au mwenye kuruhusiwa.

132.-(1) Mwenye kukubali stakabadhi ya malipo hatoruhusiwa kukataa kwamba mtoaji alikuwa na mamlaka ya kutoa stakabadhi hiyo au kuiambatanisha, ukizingatia kwamba, mpokeaji wa stakabadhi ya malipo anaweza kuikataa stakabadhi hiyo iliyotolewa na mtu ambae alitakiwa kuitoa.

(2) Mdhaminiwa au aliyeruhusiwa, hatoruhusiwa kukataa kwamba mdhamini wake au aliyempa ruhusa alikuwa na mamlaka kwa muda wakati udhamini au ruhusa ilipoanza, kufanya udhamini huo au kutoa ruhusa hiyo, kwa kuzingatia kwamba, kama mdhaminiwa atapeleka bidhaa iliodhaminiwa kwa mtu asiye kuwa mdhamini, anaweza kuthibitisha kwamba mtu huyo alikuwa na haki kwao dhidi ya mdhamini.

SEHEMU YA KUMI NA NANE
MASHAHIDI

Nani anaweza kutoa ushahidi

133.(1) Watu wote watakuwa na uwezo wa kutoa ushahidi isipokuwa Mahakama ikiona kwamba wanazuilika kutokana na kuelewa masuala wanayoulizwa, au kutoa majibu ya msingi ya maswali hayo, kwa umri mdogo, uzee sana, maradhi yakiwa ya kimwili au ya kiakili, au sababu nyengine yoyote ya aina hiyo.

(2) Mgonjwa wa akili sio kwamba hawezi kutoa ushahidi, isipokuwa anazuilika kwa sababu ya ugonjwa huo wa akili kutokana na uelewa wa maswali anayoulizwa na kutoa majibu ya msingi kwayo.

(3) Pale ambapo katika mwenendo wowote wa kesi ya jinai au jambo, mtoto mwenye umri mdogo aliyeitwa kama shahidi, kwa maoni ya Mahakama, haelewi maana ya kiapo, ushahidi wake unaweza kupokelewa ingawa, haukutolewa kwa kiapo au kwa kuthibitisha, ikiwa kwa maoni ya Mahakama ambayo yatarikodiwa katika mwenendo wa kesi, ana uelewa wa kutosha wa kuhalalisha kupokelewa ushahidi wake, na anafahamu wajibu wa kusema kweli.

(4) Bila kujali kanuni yoyote ya sheria, au uzoefu ulio kinyume chake, lakini kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (7) cha kifungu hiki, endapo ushahidi uliopokelewa kwa kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki umetolewa kwa niaba ya upande wa mashitaka na haukungwa mkono na ushahidi mwengine wowote wa maana kumuhusisha mshtakiwa, Mahakama inaweza, baada ya kujionya juu ya hatari ya kufanya hivyo kwa kutumia ushahidi huo kumtia hatiani mshtakiwa kama itathibitika kikamilifu kwamba mtoto huyo anasema ukweli.

(5) Bila kujali kanuni yoyote ya sheria, au uzoefu ulio kinyume chake, lakini kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (7) cha kifungu hiki , ushahidi wa mtoto mwenye umri mdogo utapokelewa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki unaweza kutumiwa na Mahakama kama ushahidi wa msingi wa kuunga mkono ushahidi wa mtoto

mwengine mwenye umri mdogo uliotolewa kabla au ushahidi uliotolewa na mtu mzima ambao unahitajika na sheria au uzoefu kuungwa mkono.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3), (4) na (5) cha kifungu hiki maelezo "mtoto mwenye umri mdogo" maana yake ni mtoto ambaye umri wake hauzidi miaka kumi na nne (14).

(7) Bila kujali masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki endapo katika mwenendo wa kesi za jinai zinazojumuisha makosa ya kujamiiana ushahidi pekee unaojitegemea ni wa mtoto wa umri mdogo au wa muathirika wa makosa ya kujamiiana, Mahakama itaupokea ushahidi, na baaada ya kuutathmini ukweli wa ushahidi wa mtoto wa umri mdogo au wa muathirika wa makosa ya kujamiiana, kama hali itakavyokuwa, kwa sababu zake yenyewe, bila ya kujali kwamba ushahidi huo haukuungwa mkono, itaendelea kumtia hatiani, kama sababu zilirekodiwa katika mwenendo wa kesi, Mahakama imejiridhisha kwamba mtoto wa umri mdogo au muathirika wa makosa ya kujamiiana hasemi chochote isipokuwa ukweli.

(8) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kosa la kujamiiana" maana yake ni makosa yoyote ya kujamiiana yaliowekwa ama katika Sheria ya Adhabu au sheria nyengine yoyote.

Mashahidi walio katika mazingira hatarishi na waliofanyiwa vitisho wanastahiki njia maalum.

134.-(1) Mahakama katika mwenendo wa kesi za jinai inaweza kuruhusu, wakati ikipokea ushahidi kutoka kwa mashahidi walio katika mazingira hatarishi au vitisho, kutumia njia maalum.

(2) Katika kifungu hiki shahidi aliye katika mazingira hatarishi au anaetishwa maana yake ni:

(a) mtoto;

(b) mtu mwenye mapungufu makubwa ya ufahamu na kuchanganyikiwa (asiyekuwa na uwezo wa kujifunza);

(c) mtu mwenye ugonjwa wa akili;

(d) mtu mwenye ulemavu wa viungo na uziwi; au

(e) mtu mwenye msongo wa mawazo uliotokana na uhalifu au vitisho.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki na kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, njia maalumu inajumuisha:

(a) kutokuonekana kwa shahidi na mshitakiwa;

(b) ushahidi wa moja kwa moja kwa njia ya mtandao;

(c) ushahidi uliotolewa kwa njia ya siri;

(d) kuondolewa kwa magauni;

(e) ushahidi uliorekodiwa kwa njia ya video katika mahojiano makuu;

(f) mahojiano ya upande kinzani au mahojiano rejea yaliyorikodiwa kwa njia ya video; au

(g) mahojiano na shahidi kwa kupitia mtu wa tatu; au

(h) msaada wa mawasiliano.

Shahidi bubu au kiziwi.

135. Shahidi ambae hana uwezo wa kuongea au kusikia anaweza kutoa ushahidi wake kwa njia nyengine yoyote ambayo itamfanya aeleweke, kama ni kwa maandishi, alama au kwa ishara, lakini maandishi hayo lazima yaandikwe na ishara zifanywe katika Mahakama ya wazi, ushahidi huo uliotolewa utajulikana kama ni ushahidi wa mdomo.

Wadaawa katika kesi ya madai na wake zao au waume zao.

136.-(1) Katika mienendo yote ya kesi za madai wadaawa wa kesi na mume au mke wa mdaawa yeyote katika kesi watakuwa mashahidi wanaaofaa kutoa ushahidi.

(2) Katika mwenendo wa kesi za jinai dhidi ya mtu yeyote, mume au mke wa mtu huyo, vyovyote itakavyokuwa atafaa kuwa shahidi.

Jaji na Mahakimu.

137. Jaji au Hakimu hawataweza, isipokuwa kwa amri maalum ya baadhi ya Mahakama ambayo ipo chini yake, kulazimishwa kujibu maswali yoyote yanayohusiana na tendo lake ndani ya Mahakama kama Jaji huyo au Hakimu au kwa jambo lolote ambalo alilitambua katika Mahakama kama Jaji au Hakimu, lakini anaweza kuulizwa kuhojiwa kwa mambo mengine amabayo yalitokea mbele yake wakati alipokuwa akifanya hivyo.

Mawasiliano wakati wa ndoa.

138. Hakuna mtu yeyote ambae ni au alikuwa katika ndoa atalazimishwa kuweka wazi mawasiliano yeyote yaliyofaywa kwake wakati wa ndoa na mtu yeyote ambae ni au aliyeoana nae na hatoruhusiwa kuweka wazi mawasiliano yoyote hayo mpaka mtu aliyeyafanya au wakala wake kimaslahi, ameridhia isipokuwa katika kesi baina ya watu waliooana au mwenendo wa kesi ambao mmoja wa wana ndoa ameshitakiwa kwa kosa lolote la jinai lililofanywa dhidi yake.

Ushahidi unaohusu masuala ya Dola.

139. Mtu hataruhusiwa kutoa ushahidi alioupata kutoka katika kumbukumbu rasmi ambazo hazijachapishwa, zinahusiana na masuala yoyote ya Dola, isipokuwa kwa ruhusa ya afisa mkuu wa idara husika, ambae atatoa au atazuia ruhusa hiyo kama atakavyoona inafaa.

Afisa kuhusiana na masuala ya Dola.

140. Afisa wa umma hatalazimishwa kuweka wazi mawasiliano yaliyofanywa kwake ambayo ni ya siri ya kiofisi pale ambapo ataona kwamba maslahi ya umma yataathirika kwa kubainisha huko.

Taarifa zinazohusiana na utendaji wa makosa.

141.-(1) Hakimu, Muendesha Mashtaka, Mpelelezi au Afisa wa Polisi hatalazimishwa kusema wapi alipozipata taarifa zozote zinazotokana na utendaji wa kosa lolote, na afisa mapato hatolazimishwa kusema wapi amepata taarifa yoyote kuhusiana na utendaji wa kosa lolote dhidi ya mapato ya umma.

(2) "Afisa mapato" katika kifungu hiki ni afisa aliyeajiriwa au anaehusiana na shughuli ya tawi lolote la mapato ya umma.

Mawasiliano ya kitaalamu.

142.-(1) Wakili au vakili hataruhusiwa katika muda wowote isipokua kwa ridhaa ya maneno ya mteja wake kutoa taarifa yoyote aliyopewa ndani ya kazi yake na kwa madhumuni ya ajira yake kama wakili au vakili, na au kwa niaba ya mteja wake au kutaja maudhui au sharti la waraka wowote ambao ameweza kuupata katika utekelezaji wa kazi zake na kwa madhumuni ya ajira yake kitaalamu, au kuweka wazi ushauri wowote aliopewa na mteja wake katika kutekeleza kazi zake kwa ajili ya ajira hiyo.

(2) Hakuna chochote ndani ya kifungu hiki kitakachozuia kuweka wazi:

(a) mawasiliano yoyote yaliyofanywa kwa madhumuni yoyote yaliyo kinyume na sheria au:

(b) tukio lolote lililoonekanwa na wakili au vakili yeyote, wakati akifanya kazi yake hiyo, kuonesha kwamba uhalifu wowote au udanganyifu umefanyika tokea alipoanza ajira yake hiyo.

(3) Haijalishi kama umakini wa wakili au vakili huyo yalielekea au hayakuelekea katika tukio hilo kwa au kwa niaba ya mteja wake.

(4) Jukumu lililotajwa ndani ya kifungu hiki linaendelea hadi baada ya kumalizika kwa ajira yake.

Kifungu cha 142 kutumika kwa wakalimani, n.k.

143. Masharti ya kifungu cha 142 cha Sheria hii yatatumika kwa wakalimani, na makarani au watumishi wa mawakili na mavakili.

Upendeleo hauondolewi kwa kujitolea kutoa ushahidi.

144. Iwapo upande wowote katika kesi ya madai unatoa ushahidi katika kesi ya madai wenyewe au vyenginevyo, kinyume chake, hatachukuliwa kuwa ameridhia au amekubaliana na utoaji wa taarifa huo kama ulivyotajwa katika kifungu cha 142 cha Sheria hii, na kama mtu yeyote katika kesi ya madai au kesi ya jinai atamwita wakili au vakili huyo kama shahidi, atachukuliwa kuridhia kuwekwa bayana huko iwapo atamuuliza wakili au vakili juu ya mambo ambayo, lakini kwa swala hilo, hatakuwa na uhuru wa kuweka bayana.

Mawasiliano ya siri na washauri wa kisheria.

145. Mtu hatalazimishwa kubainisha Mahakamani mawasiliano yoyote ya siri yaliyofanyika baina yake na mshauri wake wa kisheria, isipokuwa kama amejitolea mwenyewe kama shahidi ambapo atalazimika kuweka bayana mawasiliano yoyote hayo kama itakavyoonekana na Mahakama na ni muhimu kujulikanwa ili kueleza ushahidi wowote ambao ameutoa, lakini sio mengineo.

Kutoa waraka wa shahidi ambae si mdaawa.

146. Shahidi ambae si mdaawa katika kesi ya madai hatalazimishwa kutoa waraka wake wa mali yoyote au waraka wowote ambao anashikilia mali yoyote kama rehani au wakara wowote ambao kuutoa utaletea kumtia hatiani, isipokua amekubali kwa maandishi kuzitoa kwa mtu anaeomba kutolewa kwa nyaraka hizo au mtu mwengine ambae anaelalamikia.

Utoaji wa nyaraka au kumbukumbu za kielektroniki ambao mwengine mwenye kuzishikilia angekataa kuzitoa.

147. Mtu hatalazimishwa kutoa nyaraka zilizo katika himaya yake au kumbukumbu za kielektroniki zilizo katika udhibiti wake ambazo mtu mwengine yeyote angestahili kukataa kuzitoa iwapo zilikuwa katika himaya au udhibiti wake, isipokuwa mtu huyo aliyetajwa mwisho anaridhia kutolewa kwake.

Shahidi hasameheki kujibu kwa msingi kwamba jibu litamfanya kuwa na hatia.

148.-(1) Shahidi hatasameheka kujibu suali lolote kuhusiana na jambo lolote husika ambalo linabishaniwa katika shauri lolote au katika kesi ya madai au mwenendo wa madai wowote kwa msingi kwamba jibu la swali hilo lingemtia hatiani, au linaweza kuletea moja kwa moja au vyenginevyo kuwa na jukumu la jinai kwa shahidi huyo au kwamba litamfichua au linaletea moja kwa moja au vyenginevyo kumtia hatiani shahidi huyo, au kwamba litafichua au kuletea moja kwa moja au vyenginevyo kufichua shahidi huyo kwa adhabu au kutaifisha kwa aina yoyote.

(2) Jibu ambalo shahidi atalazimishwa kulitoa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, halitomfanya kukamatwa kokote au kushtakiwa au kuthibitishwa dhidi yake katika mwendeko wowote wa kesi ya jinai isipokua shtaka la kutoa ushahihi wa uongo kwa jibu hilo.

Mshiriki wa kosa.

149. Mshiriki wa kosa atakua ni shahidi anaefaa dhidi ya mshitakiwa; na kutiwa hatiani hakutokuwa batili kwa sababu pekee kuendelea kwa ushahidi usioungwa mkono kwa ushahidi wa mshiriki wa kosa.

Idadi ya mashahidi.

150. Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Adhabu au Sheria nyengine yoyote inayotumika hakuna idadi maalum ya mashahidi itakayohitajika katika kesi yoyote kwa kuthibitishwa kwa tukio lolote.

SEHEMU YA KUMI NA TISA
MAHOJIANO NA MASHAHIDI

Utaratibu wa kuwaita na kuwahoji mashahidi.

151. Utaratibu ambao mashahidi wanaitwa na kuhojiwa utaratibiwa na sheria na uzoefu uliopo kuhusiana na utaratibu wa mwenendo wa madai na jinai husika, na iwapo hakuna sheria yoyote kwa uwezo wa Mahakama.

Mahakama kuamua kuhusu kukubalika kwa ushahidi.

152.-(1) Iwapo upande wowote unapendekeza kutoa ushahidi wa tukio lolote, Mahakama inaweza kuuliza upande unaopendekeza kutoa ushahidi kwa namna gani tukio linalodaiwa, iwapo litathibitika, lingehusiana, na Mahakama itapokea ushahidi huo iwapo itaona kwamba tukio hilo, likithibitishwa, lingekuwa linahusiana na si vyenginevyo.

(2) Ikiwa tukio linalopendekezwa kuthibitishwa ni moja ambalo ushahidi unakubalika tu kutokana na uthibitisho wa tukio jengine, tukio hilo litakalotajwa mwisho lazima lithibitishwe kabla ushahidi haujatolewa wa tukio lililotajwa mwanzo, isipokuwa upande huo unataka kutoa uthibitisho wa tukio hilo na Mahakama ikaridhika na utolewaji wa uthibitisho huo.

(3) Ikiwa kuhusika kwa tukio moja linalodaiwa linategemea tukio jengine linalodaiwa lililothibitishwa, Mahakama, inaweza kwa uwezo wake ama kuruhusu ushahidi wa tukio la mwazo kutolewa kabla tukio la pili kuthibitishwa, au inaweza kutaka ushahidi kutolewa wa tukio la pili kabla ya kutoa ushahidi wa tukio la kwanza.

Mahojiano makuu, mahojiano kinzani na mahojiano rejea.

153.-(1) Mahojiano ya shahidi kwa mdaawa anaemuita yataitwa mahojiano makuu.

(2) Mahojiano ya shahidi wa mdaawa kinzani yataitwa mahojiano kinzani.

(3) Mahojiano ya shahidi baada ya mahojiano kinzani kwa mdaawa aliemuita, yataitwa mahojiano rejea.

Utaratibu wa mahojiano na maelekezo ya mahojiano rejea.

154.-(1) Mashahidi kwanza watafanyiwa mahojiano makuu, baadae, iwapo upande kinzani utahitaji, mahojiano kinzani, baadae, ikiwa upande uliomuita shahidi huyo utahitaji, mahojiano rejea.

(2) Mahojiano na mahojiano kinzani lazima yahusiane na matukio lakini mahojiano kinzani hayahitaji kufungika na matukio ambayo shahidi ameyatolea ushahidi katika mahojiano yake makuu.

(3) Mahojiano rejea yataelekezwa kwa maelezo ya mambo yaliyotajwa katika mahojiano kinzani; na iwapo jambo jipya limejitokeza, kwa ruhusa ya Mahakama, limetolewa katika mahojiano rejea, upande kinzani unaweza kuendeleza mahojiano kinzani kuhusiana na jambo hilo.

Mahojiano kinzani ya mtu aliyeitwa kutoa waraka.

155. Mtu aliyeitwa kutoa waraka hawi shahidi kwa kutoa kwake waraka huo na hawezi kufanyiwa mahojiano kinzani isipokuwa na mpaka awe ameitwa kama mashahidi.

Shahidi kuhusiana na tabia.

156. Shahidi kuhusiana na tabia anaweza kufanyiwa mahojiano kinzani na mahojiano rejea.

Maswali ya kuongoza.

157. Swali lolote linaloelekeza jawabu ambalo mtu aliyeliuliza anataka au anategemea kupokea linaitwa swali la kuongoza.

Wakati gani maswali ya kuongoza yanaweza kuulizwa.

158.-(1) Maswali yakuongoza, iwapo yatapingwa na upande kinzani, hayataulizwa katika mahojiano makuu, au katika mahojiano rejea isipokuwa kwa ruhusa ya Mahakama.

(2) Mahakama itaruhusu maswali ya kuongoza kwa mambo ambayo ni ya utambulisho au yasiyopingwa, au ambayo kwa maoni yake, yameshathibitishwa vya kutosha.

Wakati gani maswali ya kuongoza hayataulizwa.

159. Maswali ya kuongoza yanaweza kuulizwa katika mahojiano kinzani.

Ushahidi kuhusiana na mambo yaliyo katika maandishi.

160.(1) Shahidi yeyote anaweza kuulizwa, akiwa katika mahojiano, ama katika mkataba wowote, utoaji au uhaulishaji mwengine wa mali, ambayo anautolea ushahidi, hakimo katika waraka, na ikiwa anasema kwamba ulikuwemo, au kama anataka kutoa taarifa yoyote ya kuwepo maudhui waraka wowote, ambao, kwa maoni ya Mahakama, unapaswa kutolewa, upande kinzani unaweza kupinga ushahidi huo kutolewa mpaka waraka huo utolewe, au mpaka matukio yamethibitishwa ambayo yanayowajibikia upande uliomwita shahidi huyo kutoka ushahidi usio halisi wa jambo hilo.

(2) Shahidi anaweza kutoa ushahidi wa mdomo wa maelezo yaliyofanywa na watu wengine kuhusu maudhui ya nyaraka iwapo maelezo hayo yenyewe ni matukio husika.

Mahojianio kinzani kuhusiana na maelezao ya maandishi yaliyopita.

161. Shahidi anaweza kufanyiwa mahojiano kinzani kuhusiana na maelezo yaliyopita yaliyofanywa na yeye kwa maandishi au kupunguzwa kwa njia ya maandishi na ambayo yanahusiana na mambo yanayobishaniwa, bila maandishi kuonyeshwa nae, au kuthibitishwa lakini, kama ilikusudiwa kupingana naye kwa maandishi, umakini wake lazima kabla ya maandishi kuweza kuthibitishwa, kuitwa kwa zile sehemu za maandishi yake ambazo zingetumika kwa madhumuni ya kupingana naye.

Maswali halali katika mahojiano kinzani.

162. Wakati wa mahojiano kinzani, shahidi anaweza, pamoja na maswali yaliyotajwa hapo kabla, kuulizwa swali lolote ambalo linapelekea:

(a) kuujaribu ukweli wa shahidi huyo;

(b) kugundua ni nani na nafasi ipi ya shahidi huyo ni hai; au

(c) kutikisa ukweli, kwa kuharibu tabia, ingawa jibu kwa swali hilo linazusha au linapelekea kumfichua shahidi huyo na adhabu au kufilisi.

Wakati gani shahidi atalazimishwa kujibu.

163. Iwapo swali lolote kuhusiana na jambo husika katika shauri au mwenendo wa kesi, masharti ya kifungu cha 148 cha Sheria hii yatatumika.

Mahakama kuamua wakati gani swali litaulizwa na wakati gani shahidi atalazimika kulijibu.

164.-(1) Ikiwa swali lolote lile linahusiana na mambo ambayo hayahusiki na shauri au mwenendo wa kesi, isipokuwa pale ambapo inaathiri ukweli wa shahidi kwa kuharibu tabia yake, Mahakama itaamua ama shahidi atalazimishwa kujibu maswali au la, na inaweza, ikiwa itaona inafaa inaweza kumuonya shahidi kwamba hawajibiki kulijibu.

(2) Katika kutekeleza uwezo wake chini ya kifungu kidogo (1) Mahakama itazingatia mambo yafuatayo:

(a) maswali hayo ni sahihi ikiwa ni ya aina ambayo ukweli wa shutuma uliosambazwa kwa wakati huo ingeathiri maoni ya Mahakama kuhusiana na ukweli wa shahidi wa jambo ambalo analitolea ushahidi;

(b) maswala hayo si sahihi iwapo shutuma iliyosambazwa inahusu mambo mepesi sana kwa wakati huo, au ya tabia hiyo ambayo ukweli wa shutuma hiyo haujaathiri, au ungeathiri kwa kiwango kidogo, maoni ya Mahakama kuhusiana na ukweli wa shahidi wa jambo hilo ambalo shahidi analitolea ushahidi;

(c) maswali hayo si sahihi iwapo hakuna uwiano mkubwa baina ya shutuma ya tabia ya shahidi na umuhimu wa ushahidi wake;

(d) Mahakama inaweza, kama itaona inafaa, kuchukulia shahidi kukataa kwake kujibu, hisia ya kwamba jibu kama lingetolewa lisingependeza.

Swali kutokuulizwa bila ya sababu ya msingi.

165. Hakuna swali kama lilivyotajwa katika kifungu cha 164 cha Sheria hii litapaswa kuulizwa, isipokuwa mtu atakayeuliza swala hilo ana sababu za msingi za kufikiria kwamba shutuma iliyosambazwa ni kweli ipo.

Utaratibu wa Mahakama iwapo swali limeulizwa bila ya sababu za msingi.

166. Ikiwa Mahakama ina maoni kwamba swali lolote limeulizwa bila ya sababu za msingi, kama limeulizwa na wakili au vakili yeyote, kuwasilisha mazingira ya kesi mbele ya Mahakama Kuu au Mamlaka nyengine ambayo wakili au vakili huyo anapaswa katika kutekeleza fani yake.

Maswali ya kuvunja heshima na yanayokashifu.

167. Mahakama inaweza kukataza maswali yoyote au mahojiano yoyote ambayo inayaona hayana murua au ya kashfa, japo kuwa masuala au mahojiano hayo yanaweza kuwa na maslahi kwa swali hilo mbele ya Mahakama, isipokuwa yanahusu matukio yanayobishaniwa, au mambo muhimu yakujulikana ili kuamua kuwepo au kutokuwepo kwa matukio yanayobishaniwa.

Maswali yaliyokusudiwa kutusi au kuudhi.

168. Mahakama inaweza kukataza suala lolote linaloona linakusudiwa kutusi au kuudhi, au ambalo, ingawa lenyewe ni sahihi lakini Mahakamani italiona jambo hili ni la kumkosea mtu.

Uondoaji wa ushahidi hupinga majibu kwa maswali yanayothibitisha ukweli.

169.-(1) Wakati shahidi ameuulizwa na amejibu swali lolote ambalo linahusiana na uchunguzi tu kiasi linalenga kutikisha ukweli wake kwa kuharibu tabia yake, hakuna ushahidi utakaotolewa kupingana naye, lakini, ikiwa atajibu uongo, anaweza baadae kushtakiwa kwa kutoa ushahidi wa uongo.

(2) Ikiwa shahidi anaulizwa kama aliwahi kutiwa hatiani hapo kabla kwa kosa lolote la jinai na anakanusha, ushahidi unaweza kutolewa wa kutiwa kwake hatiani kwa makosa ya zamani.

(3) Ikiwa shahidi ameulizwa swali lolote linalompelekea kukanusha kutopendelea na kujibu swali hilo kwa kukataa matukio yaliyopendekezwa anaweza kupingwa.

Swali kwa mdaawa kwa shahidi wake mwenyewe.

170. Mahakama inaweza, kwa uwezo wake, kuruhusu mtu anayeita shahidi kuuliza maswali yoyote kwa shahidi huyo ambayo yangeweza kuwekwa katika mahojiano kinzani kwa upande kinzani.

Kukanusha ukweli wa shahidi.

171.-(1) Ukweli wa shahidi unaweza kukanushwa kwa njia zifuatazo kwa upande kinzani, au kwa idhini ya Mahakama, kwa upande uliomwita shahidi huyo kwa:

(a) ushahidi wa watu ambao wametoa ushahidi kwamba kutokana na uelewa wao wa shahidi, wanamuamini kwamba hana ukweli;

(b) uthibitisho kwamba shahidi alipewa rushwa au amepokea ahadi ya rushwa, au amepokea ushawishi wowote wa rushwa kutoa ushahidi wake; au

(c) uthibitisho wa maelezo yaliyopita, kupingana na sehemu yoyote ya ushahidi wake ambao unapaswa kupingwa.

(2) Shahidi anaemtaja shahidi mwengine kuwa si mkweli hawezi katika mahojiano yake makuu, kutoa sababu kwa kuamini kwake, lakini anaweza kuulizwa sababu zake katika mahojiano kinzani, na majibu anayoyatoa hayaweza kupingwa, ingawa, iwapo ni ya uongo, anaweza baadae kushtakiwa kwa kosa la kutoa ushahidi wa uongo.

Maswali yanayohitaji kuungwa mkono na ushahidi wa matukio husika yanakubalika.

172. Wakati shahidi anaekusudiwa kukuunga mkono anatoa ushahidi wa tukio lolote husika anaweza kuulizwa juu ya mazingira mengine yoyote ambayo aliyaona wakati au karibu na wakati au mahala ambapo tukio hilo husika limetokea, ikiwa Mahakama ina maoni kwamba mazingira hayo yakithibitika, yangeunga mkono ushahidi wa shahidi huyo kuhusiana na tukio husika ambalo analitolea ushahidi.

Maelezo ya nyuma ya shahidi yanaweza kuthibitishwa kuunga mkono ushahidi wa baadae kwa tukio lile lile.

173. Ili kuunga mkono ushahidi wa shahidi, maelezo yoyote ya nyuma yaliyofanywa na shahidi huyo kuhusiana na tukio lile lile wakati ambapo tukio hilo lilitokea, au kabla ya mamlaka yoyote ya kisheria yenye uwezo wa kuchunguza tukio hilo linaweza kuthibitishwa.

Mambo gani yanayoweza kuthibitishwa kuhusiana na taarifa husika zilizothibitishwa chini ya Kifungu cha 32 au 36.

174. Wakati maelezo yote husika chini ya kifungu cha 32 au 36 cha Sheria hii yamethibitishwa, mambo yote yanaweza kuthibitishwa ama ili kupinzana au kuunga mkono, au kukanusha au kuthibitisha ukweli wa mtu ambae ulifanywa kwake, ambayo ingepaswa kuthibitishwa iwapo mtu yule angeitwa kama shahidi na angekanusha katika mahojiano kinzani ukweli wa mambo yaliyoelekezwa.

Kujikumbusha na wakati shahidi anaweza kutumia nakla ya waraka kujikumbusha.

175.-(1) Shahidi anaweza, akiwa katika mahojiano, kujikumbusha kwa kupitia maandishi yoyote yaliyoyafanywa na yeye binafsi wakati tendo linalohusika ambalo linauliziwa, au mara baadae iwapo Mahakama itaona tendo hilo kwa wakati huo lilikuwa limo katika kumbukumbu zake.

(2) Shahidi pia anaweza kufanya rejea kwa maandishi yoyote yale yaliyofanywa na mtu mwengine yeyote, na kusomwa na shahidi ndani ya muda uliotajwa, ikiwa wakati wa kuyasoma alijua kwamba ni sahihi.

(3) Wakati wowote shahidi anaweza kujikumbusha kwa kufanya rejea kwa waraka wowote, anaweza, kwa ruhusa ya Mahakama, kufanya rejea ya nakla ya waraka hiyo, isipokuwa kwamba Mahakama imeridhika kwamba kuna sababu za kutosha za kutotolewa kwa waraka halisi.

(4) Mtaalam anaweza kujikumbusha kwa kufanya rejea kwenye Mikataba ya kimataifa ya kitaalamu.

Ushahidi kwa matukio yaliyotajwa katika waraka iliyotajwa katika kifungu cha 175.

176. Shahidi anaweza pia kutoa ushahidi kwa matukio yaliyotajwa katika waraka wowote ule kama ilivyotajwa katika kifungu cha 175 cha Sheria hii, ingawa hana mkusanyiko maalum wa matukio yenyewe, iwapo ana uhakika kwamba matukio hayo yalirikodiwa kwa usahihi katika waraka.

Haki ya upande kinzani kuhusiana na maandishi yaliyotumika kujikumbushia.

177. Muandiko wowote uliotajwa chini ya masharti ya vifungu 175 na 176 vya Sheria hii yatatolewa na kuonyeshwa kwa upande kinzani ikiwa atayahitaji; upande huo ikiwa utapenda, unaweza kumfanyia shahidi mahojiano kinzani.

Kutolewa kwa nyaraka na tafsiri ya nyaraka.

178.-(1) Shahidi aliyeitwa kutoa waraka, ikiwa uko katika himaya au udhibiti wake atalazimika kuuleta Mahakamani, bila ya kujali pingamizi yoyote inayoweza kuwepo kwa kutolewa kwake au kukubalika kwake.

(2) Uhalali wa pingamizi yoyote ilio chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utaamuliwa na Mahakama.

(3) Mahakama, ikiona inafaa, inaweza kukagua waraka, isipokuwa kama inahusu mambo ya Dola, au kuchukua ushahidi mwengine kuiwezesha kuamua juu ya kukubalika kwake.

(4) Ikiwa kwa madhumuni hayo ni muhimu waraka wowote kutafsiriwa, Mahakama inaweza, ikiona inafaa, kuelekeza mwenye kutafsiri kuweka siri ya maudhui yake, mpaka nyaraka itolewe ushahidi na, ikiwa mtafsiri hatokubaliana na isipokuwa kama waraka huo unapaswa kutolewa kama ushahidi; na ikiwa mwenye kutafsiri hatotii maelekezo hayo, atakuwa amefanya kosa la kudharau ofisi linalohukumiwa kwa mujibu wa Sheria husika.

Kutoa, kama ushahidi wa waraka ulioitwa kwa, na kutolewa kwa notisi.

179. Wakati mdaawa anataka kutolewa kwa waraka ambao ametoa notisi ya kutolewa kwa upande mwengine na waraka huo umetolewa na kukaguliwa na upande uliotaka utolewe, anapaswa kuutoa kama ushahidi ikiwa upande ulioutoa utamtaka kufanya hivyo.

Kutumia, kama ushahidi, wa utoaji waraka ambao ulikataliwa kwa notisi.

180. Ikiwa mdaawa anakataa kutoa waraka ambayo ana notisi ya kuutoa, hapo baadae hawezi kuutumia waraka huo kama ushahidi bila ya ruhusa ya upande mwengine au amri ya Mahakama.

Uwezo wa Mahkama kuuliza maswali au amri ya utowaji.

181.-(1) Jaji au Hakimu anaweza, ili kugundua au kupata uthibitisho sahihi wa matukio husika, kuuliza suali lolote husika kuhusiana na tukio lolote na anaweza kuamuru utowaji wa waraka wowote au kitu.

(2) Hukumu lazima iegemee kwenye matukio yaliyotamkwa na Sheria hii kuwa ni husika, na kuthibitika ipasavyo.

(3) Kifungu hiki hakitomuidhinisha Jaji au Hakimu yeyote kumlazimisha Shahidi yoyote kujibu swali lolote, au kutoa waraka wowote ambao shahidi huyo angepaswa kukataa kujibu au kutoa kwa mujibu vifungu vya 137 hadi 147 vya Sheria hii, vyote kwa pamoja, ikiwa swali liliulizwa au waraka uliitishwa na upande kinzani; hakuna Jaji au Hakimu ambae atauliza swali lolote ambalo lisingekuwa sahihi kwa mtu mwengine yeyote kuuliza chini ya kifungu 165 au 166; wala hatotoa ushahidi halisi wa waraka wowote, isipokuwa katika mazingira yaliyotengwa humu.

Uwezo wa washauri wa Mahakama kuuliza maswali.

182. Katika kesi zinazosikilizwa pamoja na washauri wa Mahakama washauri hao wanaweza kuuliza maswali yoyote kwa mashahidi kupitia au kwa ruhusa ya Jaji, ambayo Jaji mwenyewe angepaswa kuyauliza na ambayo anaoona yanafaa.

SEHEMU YA ISHIRINI
KUKUBALI KUSIKO SAHIHI NA KUKATALIWA USHAHIDI

Hakuna kusikilizwa upya kwa kukubaliwa kusiko sahihi au kukataliwa ushahidi.

183. Kukubaliwa kusiko sahihi au kukataliwa kwa ushahidi kwenyewe haitokuwa sababu ya msingi ya kusikilizwa upya au kubatilishwa kwa maamuzi yoyote katika kesi yoyote, ikiwa itatokea kwa Mahakama ambayo pingamizi hiyo imezushwa kwamba, kujitegemea kwa ushahidi huo kunapingwa na kupokelewa, kulikuwa na ushahidi wa kutosha kuhalalisha uamuzi, au kwamba, ikiwa ushahidi uliokataliwa umepokelewa, haipaswi kubatilishwa uamuzi huo.

Uwezo wa kutunga kanuni.

184.-(1) Jaji Mkuu anaweza kutunga kanuni ili kutekeleza masharti ya Sheria hii.

(2) Hasa, na bila yakukiuka uwezo wa jumla uliotajwa, kanuni hizo zinaweza kuweka yote au lolote ya mambo yafuatayo:

(a) namna ambayo taarifa au jambo lolote linaweza kuthibitishwa kwa njia ya saini ya kidigitali;

(b) namna na muundo ambo kumbukumbu za kieletroniki zitawasilishwa, au kutolewa Mahakamani;

(c) mambo yanayohusiana na aina ya saini ya kidigitali, namna na muundo ambao unaweza kuwekwa;

(d) taratibu za kiusalama kwa madhumuni ya kupata kumbukumbu salama za kieletroniki na saini salama ya kidigitali;

(e) jambo jengine lolote linalotakiwa kufanywa au linaloweza kuelezwa.

(3) Kila kanuni inayofanywa na Jaji Mkuu chini ya kifungu hiki itatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kufuta na kuhifadhi.

185.-(1) Sheria ya Ushahidi Sura ya 5 inafutwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Ushahidi Sura ya 5, kesi zote zilizoanza kabla ya kufutwa kwa sheria hiyo zitaendelea chini ya utaratibu wa Sheria iliyofutwa.

Umepitishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 23 Novemba, 2016.

RAYA ISSA MSELLEM
KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR